**Nipashe**

Jumatatu Aprili 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581640

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



UKURASA 11

**MECHI BORA ZA EPL MAN UTD, LIVERPOOL**

**Wawili** wafariki dunia mtumbwi ukipinduka mtoni

UKURASA 17

**Nchimbi:** Viongozi wote waombewe kutimiza wajibu

UKURASA 18



**Makonda** asubiriwa kubadili Arusha sekta ya utalii

UKURASA 3

# MAJANGA SHULENI

• **Wanafunzi**, walimu wajisaidia vichakani kwa miaka mitatu... *Endelea Ukurasa 2*



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi wakiongoza viongozi mbalimbali katika dua mbele ya kaburi la Hayati Sheikh Abeid Amani Karume katika kumbukizi ya miaka 52 ya kifo chake, iliyofanyika Ofisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kisiwandui, Zanzibar jana. **PICHA: OMR**

## Wiki ngumu kwa vigogo serikalini, hoja tisa zasubiri kauli ya PM

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wakishuhudia Rais wa Rwanda, Paul Kagame akiwasha mwenge wakati wa maadhimisho ya miaka 30 ya kumbukumbu ya mauaji ya Kimbari, jijini Kigali, Rwanda jana. **PICHA: IKULU**

LICHA YA KATAZO

## Viwanja vya mita 20 kwa 20 vyaliza mijini

UKURASA 4

**MICHEZO** GAMONDI MGUU NJE NDANI YANGA UK.24

**MAONI,** UK.6



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, SACP Agustino Senga, akitoa elimu kuhusu madhara ya ukatili na uhalifu yanayotokea katika jamii, alipohudhuria ibada ya Jumapili katika Kanisa la Moraviani la Majengo, mjini Tunduma wilayani Momba jana. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

MAJANGA SHULENI

# Wanafunzi, walimu wajisaidia vichakani

**Na Waandishi Wetu,** SONGEA

BAADHI ya wazazi wa wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Tembo Mashujaa, mjini Songea wametishia kutorejesha shuleni watoto wao kutokana na choo cha wanafunzi shuleni huko kujaa.

Hiyo ni shule ya serikali, iliyoko chini ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma. Iliko ni umbali wa kilomita 3.8 kutoka katikati ya mji wa Songea. Kwa usafiri wa umma, nauli yake ni Sh. 500 kwa daladala au bajaji.

Ni vigumu kubaini kuwapo shule katika eneo hilo kutokana na kuzungukwa na mandhari tulivu ya kijani na yenye miti. Imo ndani ya Brigedi ya Tembo, Songea.

Choo cha wanafunzi kimejaa, waandishi wa habari hizi wameshuhudia. Wanafunzi wanaosomea shuleni huko ni takribani 800 wanaofundishwa na walimu 17, kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mary Mpyambala. Matundu ya choo ni 10; matano kwa ajili ya wavulana na mengine kwa ajili ya dada zao.

Wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo wameuomba uongozi wa wilaya kunusuru watoto wao dhidi ya hatari ya choo hicho kujaa na kuweka rehani afya na maisha ya wanafunzi na walimu.

Kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, wazazi hao, akiwamo Lucas Komba, mkazi wa eneo la Bombambili, mjini Songea, walisema hali ya mazingira katika shule hiyo ni mbaya, kwa kuwa ni muda mrefu umepita tangu choo kijae.

"Kama wazazi tumejitahidi sana kuhamasishana kuchangia fedha, ili kuona namna ya kujenga choo, lakini imekuwa ngumu, kwa sababu fedha kidogo ambazo zilipatikana zilielekezwa kwenye chakula cha mchana kwa wanafunzi.

"Fedha zilielekezwa kwenye chakula kwa madai kwamba serikali ina fedha, itajenga choo. Jambo ambalo limekuwa ni kitendawili hadi leo. Ni tatizo la muda mrefu, hakuna suluhisho," alisema Komba.

Elisha Ndunguru, mkazi wa Making'inda, Kata ya Msamala, mjini hapa, alisema wazazi wana hofu kuhusu afya za watoto wao wanaosoma katika shule hiyo, hivyo wanamwomba Mkuu wa Wilaya ya Songea, Kapenjama Ndile, kusaidia ujenzi wa choo utekelezwe haraka shuleni huko.

Alisema kama itakuwa ngumu kutekeleza ujenzi kwa muda mfupi, ni heri shule hiyo ifungwe ili kunusuru afya na maisha ya watoto wao.

Ndunguru alisema pamoja na shule hiyo kuwa katikati ya Manispaa ya Songea, ina tatizo hilo ambalo viongozi karibu wote wana taarifa zake, lakini hatua hazichukuliwi.

Alisema Kamati ya Shule hiyo iliitisha kikao na wazazi wa watoto wanaosoma shuleni huko; walikubaliana kwa pamoja "ni lazima choo cha shule kijengwe kwa kuchangishana".

Alisema, "Tulianza kuchangishana kila mwanafunzi anayesoma katika shule hii anatoa Sh. 100. Na kwa ambao wana uwezo waliambiwa watoe fedha zaidi ya hiyo, ili kufanikisha kujenga choo."

Mkazi mwingine wa eneo hilo aliyejitambulisha kwa jina la Mama Irene, alisema, "Mwaka jana Juni, kikao kilifanyika tukaongea na meya, akasema kuna Sh. milioni tano, akathibitisha, tukasema shule ikifunguliwa hatuleti watoto, akasema 'choo kitakuwa tayari'.

"Ila hadi shule inafunguliwa hamna choo. Hadi Desemba, mwaka jana, hamna choo. Sasa wazazi tumejitolea kujenga choo, Meya anasema wanaweza kujenga. Shule ilipokuwa inaanza ilikuwa na matundu 10, matumizi yameongezeka, yamejaa na kimebomoka."

**UONGOZI WA SHULE**

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Masumbuko Mbogoro, alisema mazingira ya choo ni mabaya kwa sababu matundu yote 10 yameziba na kusababisha haja kubwa kuzagaa.

Aliomba uongozi wa manispaa kuchukua hatua za haraka, kusaidia ujenzi huo kwa kuwa mvua inayoendelea kunyesha itasababisha mlipuko wa magonjwa hasa ya kuambukiza, kama vile kipindupindu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi TemboMashujaa, Mary Mpyambala, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, kuhusu tatizo hilo alithibitisha lipo kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi zaidi ya 800 ambao wengi wao wakibanwa haja, hulazimika kwenda kujisaidia porini, hivyo kuwa hatarini kupata magonjwa ya kuambukiza na kung'atwa na wadudu kama nyoka na hata kushambuliwa na wanyama wakali.

Mwalimu huyo alisema licha ya jitihada kuendelea kufanyika baina ya wazazi, uongozi wa shule na serikali kulimaliza tatizo hilo, utatuzi wake unasuasua.

Mwalimu Mkuu Mary pia alibainisha kuwa hata walimu 17 wa kike na kiume wa shule hiyo, nao wanategemea kujisitiri kwenye matundu hayo 10 ya choo yanayotumiwa na wanafunzi wa jinsi zote, ambayo yamejaa.

"Tunawekeana zamu, walimu na wanafunzi, kwenda kujisaidia kwa kuwa shule ina choo cha matundu 10. Nayo yameshajaa siku nyingi. ... (alitaja neno lenye maana ya haja kubwa) huzagaa, ni hatari kwa afya.

"Wakati mwingine hata walimu wanalazimika kwenda porini kujisaidia. Na hapa tumezingirwa na msitu wa miti ya kambi ya jeshi," alisema.

**WATENDAJI SERIKALINI**

Meya wa Halmashauri ya Songea, Michael Mbano, akizungumza na gazeti hili, alithibitisha mazingira ya choo shuleni huko si rafiki kwa wanafunzi kwa sababu kimejaa, akisisitiza hatua zinachukuliwa.

Alisema halmashauri imetenga Sh. milioni tano kwa ajili ya ujenzi wa choo, huku akiomba wazazi wa wanafunzi wanaosoma shuleni huko kuona umuhimu wa kuchangia fedha ili kufanikisha ujenzi huo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ujenzi wa tundu moja la choo unagharimu Sh. milioni 1.1, hivyo Sh. milioni tano zilizotengwa na manispaa zinatosha kujenga matundu manne tu shuleni TemboMashujaa.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Sosteness Mbwilo, alisema: "Vyoo vipo, ila vya muda mrefu, ni vya zamani, vimechakaa.

"Halmashauri imeshirikiana na wananchi kuchimba choo, ili kuanza ujenzi na fedha ikitolewa inaingia katika akaunti ya kanda. Idara ya Mipango na watendaji wa kata, wanajua hilo."

Mkuu wa Wilaya Songea, Kapenjama Ndile, alisema mwishoni mwa wiki kuwa taarifa kuhusu hali hiyo zimemfikia, hatua zimeanza kuchukuliwa kuhakikisha ujenzi wa vyoo shuleni huko unaanza.

Alisema kuwa alitembelea shuleni huko hivi karibuni, hivyo haoni sababu ya kuendelea kukaa kimya.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza kila shule iwe na vyoo kwa ajili ya wanafunzi kwa uwiano wa tundu moja kwa wavulana 25 na tundu moja kwa wasichana 20, pia kuwe na vyoo kwa ajili ya walimu wao.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Gideon Mwakanosya.**

# Wiki ngumu vigogo serikalini yawadia

## ●Hoja tisa zasubiri kauli ya Waziri Mkuu

**Augusta Njoji na Vitus Audax,** DODOMA

MKUTANO wa Bunge la Bajeti 2024/25 unaingia katika juma la pili leo, ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 zikiwasilishwa bungeni kwa mujibu wa sheria.

Ibara ya 143 ya Katiba ya nchi (1977) inaelekeza Rais baada ya kukabidhiwa taarifa ya ukaguzi wa CAG, aiwasilishe bungeni kupitia wasaidizi wake ndani ya siku saba tangu kuanza kwa mkutano unaofuata wa Bunge (siku za sikukuu na mwishoni mwa wiki hazihesabiki).

Rais Samia Suluhu Hassan alipokea ripoti za CAG Machi 28, mwaka huu. Mkutano wa Bunge ulianza Jumanne iliyopita, hivyo kuna siku tatu kuanzia leo kuwasilishwa ripoti hizo bungeni ili kukidhi matakwa ya kikatiba.

Ripoti za CAG zitakazowasilishwa bungeni ni ripoti kuu ya ukaguzi; Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu; Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama; na Ukaguzi wa Ufanisi.

Pia kuna ripoti za ukaguzi 14 katika maeneo maalum, mojawapo likiwa hali ya utoaji huduma kwa magonjwa ya akili nchini.

Kuwasilishwa kwa ripoti hiyo bungeni na hivyo kuwa wazi kwa umma, kunatarajiwa kuwa mwiba kwa baadhi ya watendaji serikalini ambao CAG Charles Kichere ameweka wazi kwamba taasisi zao zina dosari kiutendaji, ikiwamo matumizi mabaya ya fedha za umma.

Hawa ni pamoja na vigogo wa taasisi kama vile Bohari ya Dawa (MSD), Udart, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na watendaji wa halmashauri, hasa waliokula fedha mbichi, kushindwa kukusanya fedha za umma na kushindwa kutoa fungu kwa ajili ya makundi maalum.

Vilevile, kuna mashirika ambayo yanatajwa kuendelea kujiendesha kwa hasara ambayo ni pamoja na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Reli Tanzania (TRC), kampuni ya uwekezaji ya TANOIL na Shirika la Posta.

Baada ya kuwasilishwa bungeni na mawaziri husika, ripoti za CAG zitakabidhiwa kwa kamati za Bunge zenye mamlaka ya kuzifanyia uchambuzi.

Pamoja na hayo, juma hili wabunge watapata majibu ya hoja zilizoibuliwa wakati wa mjadala wa mapitio ya utekelezaji bajeti ya mwaka 2023/24 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ya 2024/25 ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake.

Hoja hizo ni pamoja na sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu, hatari ya kufilisika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutokana na serikali kuchukua fedha za mfuko Sh. bilioni 208 na kuzitumia kwenye miradi yake, adha upatikanaji mikopo ya elimu ya juu na ugumu wa upatikanaji nishati ya gesi vijijini.

Hoja zingine ni kilio dhidi ya wanyamapori hatari kwa binadamu, hasa tembo na mamba, kukithiri mikopo ya kausha damu nchini, matumizi ya shisha, madeni ya askari magereza pamoja na utitiri wa tozo katika sekta ya uvuvi.

Baada ya kuhitimishwa kwa mjadala huo, kutawasilishwa bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka 2024/25, ambayo mjadala wake umepangwa kuchukua siku tatu.

# Makonda asubiriwa kuibadili Arusha sekta utalii

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa ARUSHA



BAADHI ya wafanyabiashara mkoani hapa wamesema wanamsubiri kwa hamu Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda (pichani), kwa ajili ya kuwatatulia kero zao ikiwamo sekta ya utalii kwa madai kuwa wanaonufaika ni wageni.

Vile vile, wanasubiri kufufuliwa kwa viwanda vilivyokufa ambayo vilikuwa vinategemewa na wananchi.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Arusha leo anatarajiwa kukabidhiwa rasmi ofisi na mtangulizi wake, John Mongela.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana kwa nyakati tofauti, Askofu wa Kanisa la Kilutheri Afrika Mashariki na mfanyabiashara Dk. Philemon Mollel, maarufu Monaban alisema kwa sasa changamoto zao zitakwenda kutatuliwa kwa kuwa Makonda ni mchapakazi.

Alisema Makonda kupelekwa mkoani Arusha ni sawa na kusema kiatu kimempata mvaaji na wana imani matatizo yao yamefika mwisho.

Mollel alisema wafanyabiashara wanampokea kwa mikono miwili na kumuunga mkono na wananchi wote bila kujali itikadi zao za kisiasa wamepata sehemu ya kupeleka matatizo yao.

Alisema wafanyabiashara wanafanya kazi kwa kuitegemea serikali na wanahitaji mtu ambaye akipatiwa kero zao zitatatuliwa.

Kadhalika, alisema Arushakuna viwanda vilikuwa havijafunguliwa na sasa wana imani vinaenda kufunguliwa na fitina zote zilizokuwapo kiboko yao ni Makonda.

"Hapa Arusha hatuhitaji fitina wala ugomvi, tunahitaji amani ni sehemu ambayo watalii wapo kila siku na Arusha ni lango la mji, pakiwa na amani Tanzania nzima imekuwa na amani na mambo mengi yamekuwa yakifanyika hapa kwa kuwa tumempata Makonda," alisema Mollel.

Aidha, alisema wataendelea kuviombea vyama vya siasa kuwa na umoja na ushirikiano kwa sababu maandiko yanawataka watu wakae kwa pamoja ili Arusha iwe kitu kimoja na wapate maendeleo na kuishi kwa amani.

Mfanyabiashara Nathan Kimaro, alisema Makonda atakuwa mwarobaini wa kutatua changamoto zao zilizokuwa zikiwasumbua kwa muda mrefu.

"Mkoa wa Arusha unategemea sekta ya utalii na wanaonufaika sio Watanzania wazawa, tuna makampuni mengi ya ndani lakini wazawa hawajapata mafanikio makubwa kwa kiwango cha utalii tunamuomba Makonda ahakikishe anayanyanyua makampuni ya kitalii ndani ya mkoa huu yaweze kuwa sehemu ya keki ya taifa ya utalii," alisema.

Alisema hata vijana ambao wanawasindikiza watalii hawanufaiki na kazi wanayoifanya na kujikuta wakiendelea kuishi katika mazingira magumu.

Aidha, alisema jiji la Arusha limekosa mandhari nzuri kama ilivyo ukubwa wa jina lake kwa kuwa bado ni chafu na sekta ya madini haijaweza kunufaisha watu wengi.

"Uwapo wa thamani ya madini pale Mererani haijaakisi maisha ya Mtanzania mmoja mmoja kwa hapa Arusha sasa itakuwa vizuri soko letu la madini liwe soko la madini kimataifa wazungu waje na watu wengine ili Tanzanite iweze kuuzwa na kutusaidia sisi," alisema Kimaro.

Kimaro alisema sekta ya makazi ya kujivinjari na nyumba bado imekuwa ni changamoto kama alivyoeleza Rais Samia ni kweli ndani ya mkoa wa Arusha wakija watalii 1,000 hakuna pa kuwalaza sasa ni wakati wa Makonda kuwaleta wawekezaji kuja kujenga magorofa ya hoteli.

Alisema changamoto nyingine ni kukosekana kwa mipango mini katika jiji la Arusha kwa sababu watu wameanza kujenga kiholela wakati ni jiji la kitalii.

Naye mfanyabiashara anayechoma nyama katika eneo la Kwa Mrombo, Kata ya Murieti, Mwijuma Mbaruku, amesema wanafanya biashara zao katika mazingira magumu licha ya kulipa ushuru bila kufanyiwa maboresho kwa muda mrefu.

"Tunaomba watuwekee mifereji ya kupitisha maji haya mazingira hayavutii tuna jina kubwa na kila anayefika Arusha lazima aje kula nyama hapa kwa Mrombo hadi wazungu wanakuja ukiangalia haya mazingira hayaridhishi watuboreshee ili wanaokuja wafurahie mazingira," alisema.

Nipashe MWANGA WA JAMII
The Guardian www.ippmedia.com

## Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia wikiendi ijayo ya tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya Nipashe na The Guardian yatakuwa yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

LICHA YA KATAZO KISHERIA

# Viwanja vya mita 20 kwa 20 vyaliza mijini

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya kuwapo katazo kisheria na taaluma ya mipangomiji kuhusu kuuza viwanja vya ukubwa wa mita 20 kwa 20, biashara hiyo bado imeshamiri mijini.

Madalali wanaouza viwanja hivyo wanadai hawajui kuwapo katazo hilo, huku kukiwa na shida nyingine ya kiwanja kuuzwa kwa wateja wawili au zaidi.

Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya Mwaka 2007, Sura 355, kifungu Na. 77(1)(b)(i), pia Kanuni za Viwango vya Upimaji Maeneo (2018) vinaweka ukomo wa ukubwa wa kuanzia katika upimaji viwanja; kiwanja kidogo zaidi chenye ukubwa wa mita za mraba 400 kinapaswa kuwa katika uwiano wa upana wa mita 16 na urefu 25.

Sheria inasema "Uwiano wa moja kwa moja (mita) 20 kwa 20 haukubaliki kitaaluma."

Kukiwa na katazo hilo la kisheria, kwa nyakati tofauti katika miji mbalimbali nchini, waandishi wa habari hizi wamebaini madalali wanaendelea kuuza viwanja hivyo vya mita 20 kwa 20.

Dalali Shija Maganga, ambaye ni mkazi wa Mivumoni, mkoani Dar es Salaam, alisema viwanja vya uwiano huo wanaviuza mara nyingi na gharama zake hufikia hadi Sh. milioni 30 kwa kiwanja kulingana na eneo.

"Goba (Dar es Salaam) kiwanja cha uwiano wa mita 20 kwa 20 utauziwa hadi Sh. milioni 30 na maeneo mengine ninauza hadi Sh. milioni 20, hivyo inategemea kiwanja kipo wapi kwa kuwa sehemu nyingine unavipata kwa Sh. milioni 10.

"Mimi ninauza, hilo katazo la viwanja vya uwiano wa (mita) 20 kwa 20 sijaelewa maana hata wenyewe (Wizara ya Ardhi) wanatoa hati ya kiwanja ambacho hata hakijafika uwiano wa (mita) 20 kwa 20," alisema Maganga.

Philimon Shoo ambaye ni dalali mkoani Dar es Salaam, alisema, "Ninadhani hili katazo ni kwa wale wenye kiwanja kikubwa ambao huvikataka kwa uwiano wa mita 20 kwa 20."

Dalali wa viwanja vilivyoko maeneo ya Kisesa, mkoani Mwanza, Maneno Exavery, alisema wamekuwa wanapanga bei ya viwanja kulingana na maeneo viliko na fursa zinazopatikana katika eneo husika ikiwamo kuwapo vyuo, stendi na huduma muhimu za kijamii kama barabara na maji.

Alisema kwa maeneo ya Chuo cha Mipango Kisesa, gharama ya kiwanja cha uwiano wa mita 20 kwa 20 kinaanzia Sh. milioni nane, Nyamhongoro ya Juu Sh. milioni moja na vya ukubwa wa 40 mita kwa 40 ni Sh. milioni nne kwa maeneo ya stendi mpya ya Kayenze.

Dalali mwingine, mkazi wa Mjini Kahama, mkoani Shinyanga aliyejitambulisha kwa jina moja la Issa, alithibitisha baadhi yao kuuza viwanja kinyemela na kudai kuwa wapo wanaoshiriki vitendo hivyo kuwa kushirikiana na watumishi kutoka Idara ya Ardhi na kuomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria.

Ally Omari, dalali wa viwanja maeneo ya Nyegezi, jijini Mwanza, alithibitisha baadhi ya madalali wamekuwa wakiongeza bei ya viwanja; hata mteja akishalipa atalazimika kulipa fedha ya kuandikishana.

"Baadhi ya madalali mtaani ni matapeli, anaweza kuuza kiwanja ambacho tayari kimeshanunuliwa na mtu mwingine na mwisho wa siku mnaingia katika migogoro ya ardhi," alisema Ally.

Bakari Juma, dalali wa viwanja, nyumba na magari mkoani Arusha, alisema, "Mwananchi anakuja kununua kiwanja, lakini fedha yake ni kidogo, hivyo huwa tunapima kiwanja kulingana na kiasi cha fedha ya mteja."

**WANANCHI WALIA**

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe walilalamikia kuendelea walichokiita "kupigwa na madalali" kwa kuuziwa viwanja vya ukubwa huo hadi Sh. milioni 30 kwa kiwanja.

Mkazi wa Kata ya Nyanga, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, Jaidu Gerald, alisema baadhi ya madalali huchangia gharama za ardhi kuwa juu na kutofautiana na uhalisia huku wakiuza viwanja vidogo visivyokidhi matakwa ya kisheria.

"Hapa tunauziwa kiwanja cha kawaida kwa ajili ya kujenga nyumba, Mfano, kiwanja cha uwiano wa (mita) 20 kwa 20 unauziwa hadi Sh. milioni mbili.

"Hili linafanya wananchi wengi tushindwe kumudu gharama na kuangukia maeneo ya kubanana, unakosa hata sehemu ya kuendeleza ujenzi wako," alisema.

Lameck Burchad, mkazi wa Kata ya Kagondo, mkoani humo, alisema licha ya kuuziwa kiwanja kwa bei ghali, baadhi ya madalali wamekuwa wanasababisha migogoro.

"Unakuta kila mtu amejenga eneo lake lote, baada ya ujenzi anaanza kulumbana na jirani yake kutokana na kukosa barabara," alisema.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa

Mkazi wa Mkoa wa Arusha, Elibariki John, alisema uuzwaji viwanja vidogo kiholela bila kufuata utaratibu unaofanywa na madalali unaumiza wananchi.

"Unakuta madalali wananunua shamba kubwa halafu wanaliuza kwa vipande vidogo vya ukubwa wa mita 20 kwa 20 na kufanya maeneo mengi kutokuwa na mipango miji," alisema.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Elisante Emmanuel, alisema utaratibu huo ni unyonyaji kwa wananchi kwa kuwa mwananchi analipa kiasi kikubwa cha fedha, lakini eneo analonunua linakuwa dogo na kuchangia miji kutopangika.

**UUZAJI MARA MBILI**

Mkazi wa Nyakato, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Simon Paschal, alisema tabia ya baadhi ya madalali kuuza kiwanja kimoja mara mbili au zaidi limechangia kuwapo migogoro ya ardhi.

Alisema suala hilo linasababishwa na baadhi ya madalali wa kujitegemea ambao wanafanya kazi kwa karibu na maofisa ardhi kwa kuuza viwanja kwa watu wawili tofauti na kuchangia uporaji haki za baadhi ya wananchi kumiliki ardhi.

Alisema ili kumaliza migogoro hiyo, wizara yenye dhamana inatakiwa kupiga marufuku suala hilo na kuchukuliwa hatua dhidi ya watumishi wanaojihusisha na tabia hiyo inayoibua migogoro.

Rashid Kakinga, mkazi wa Nyasaka, mkoani Mwanza, aliomba serikali iweke bei elekezi ya viwanja kulingana na eneo na ukubwa ili kupunguza ulanguzi kwa wananchi.

"Hii itachangia wananchi wengi kumiliki ardhi na nyumba kuliko ilivyo sasa; walio wengi wanashindwa kutokana na changamoto zilizopo," alisema.

**KAULI SERIKALINI**

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangale, alikiri kuwapo migogoro hiyo inayosababishwa na baadhi ya madalali wasio waaminifu ambao mara kwa mara wamekuwa wanawaripoti katika Ofisi za Idara ya Ardhi ili wachukuliwe hatua.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mbugani, jijini Mwanza, Benedict Kabadi, alisema kwa maeneo ya mjini ni ngumu kupata malalamiko kuhusu viwanja kutokana na mazingira yalivyo kwa kuwa viwanja vyote vimepimwa na watu wamejenga.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Mwanza, Happiness Mtutwa, alisema serikali imekuwa inadhibiti mara kwa mara vitendo vya madalali wasiokuwa waaminifu wanaouza kiwanja kwa wateja zaidi ya mmoja, pia kukiuka vipimo elekezi.

Alitaja kadhia hiyo hukwamishwa na baadhi ya watumishi wa serikali, hususani maofisa watendaji, wenyeviti wa mitaa na vijiji na wengine kutoka Idara za Ardhi katika halmashauri husika.

Mtutwa alisema maeneo yote ya Mkoa wa Mwanza kuna bei elekezi ya serikali kulingana na eneo husika, lakini baadhi ya watendaji wa serikali wamekuwa wanasimamia hilo kinyume cha sheria, licha ya mamlaka ya ardhi kupiga marufuku uuzaji viwanja vya ukubwa wa mita 20 kwa 20 na usiofuata vipimo.

Kama ilivyolalamikiwa na wadau wengine waliozungumza na Nipashe, Mtutwa alisema baadhi ya watumishi wa serikali wamekuwa wanashirikiana na madalali kuuza kwa kipimo cha mita 20 kwa 20.

"Wananchi wamekuwa hawafuati taratibu za umiliki na ununuzi wa ardhi kabla ya kununua viwanja, hali ambayo hutoa mianya ya wao kutapeliwa na matokeo yake kuishia kuleta malalamiko katika ofisi zetu baada ya tatizo kuwa kubwa. Kesi hizi ni nyingi ofisini kwangu," alisema.

Aliongeza kuwa biashara holela ya viwanja inaharibu taswira na mwonekano wa miji na kusababisha mpangilio mbovu wa miji kwa kuwa wananchi wanajenga kiholela.

"Migogoro mingi ya ardhi inatokana na ukosefu wa elimu kwa wananchi na baadhi ya watumishi kukosa uzalendo katika utendaji wao wa kazi," alisema.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Masaki, Manispaa ya Kigamboni, Revocatus Mwinjukya, alisema, "Changamoto kubwa inayotukabili kwa sasa ni wananchi kuvamia maeneo ya wazi na mabonde.

"Mfano, tuna maeneo ya wazi 11 kwenye viwanja vilivyopimwa, lakini mengine yamevamiwa na watu wamejimilisha, viwanja vya uwiano wa mita 20 kwa 20 ni Sh. milioni mbili huko walikojimilikisha," alisema.

Mjumbe huyo alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa maeneo ya wazi na hatari ya kujenga bondeni.

Septemba Mosi, 2022, aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, wakati akifungua mkutano wa wadau wa uendelezaji milki, alisema uwiano wa mita 20 kwa 20 haukubaliki katika upimaji wa viwanja kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji, pia taaluma ya mipangomiji.

Alielekeza kampuni binafsi za upangaji, upimaji na zinazojihusisha na masuala ya ardhi na yeyote anayejihusisha na uuzaji wa vipande vya ardhi kwa mtindo huo, kusitisha kazi hizo na kurejesha fedha kwa wananchi kwa maeneo ambayo tayari yana migogoro.

**SHERIA INAVYOSEMA**

Katika Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya Mwaka 2007, Sura 355, Kifungu Na. 77(1)(b)(i), Kanuni ya Viwango vya Upimaji Maeneo zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 91 na 93, Machi 9, 2018, ukubwa wa maeneo kwa matumizi mbalimbali umeainishwa.

Sheria hii na taaluma ya mipangomiji inaainisha viwanja vya matumizi mbalimbali vinatakiwa kuwa na ujazo tofauti, ujazo wa juu, ujazo wa kati na ujazo wa chini.

Viwanja hivi vinatakiwa kuwa na mapana na marefu yenye uwiano wa moja kwa mbili mpaka moja na mbili na nusu. Kwa mfano, kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 400 kinapaswa kuwa katika uwiano wa upana wa mita 16 na urefu 25.

Takwimu za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zinaonesha kuwa hadi mwaka 2022, sekta ya milki ilikuwa na changamoto kadhaa ikiwamo uhaba mkubwa wa nyumba hususani zenye ubora na zile za gharama nafuu, nchi ikiwa na upungufu wa takribani nyumba milioni tatu huku kukiwa na ongezeko la mahitaji ya wastani nyumba 200,000 kwa mwaka.

HABARI KITAIFA

# Spika Tulia apongeza NMB ikifuturisha wabunge, yatima

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WIKI moja baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kupongeza Benki ya NMB kwa jicho la huruma kwa watoto yatima na kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi za fedha kujifunza kwao kuwafikia na kusaidia wenye uhitaji, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amekiri kuvutiwa na ibada hiyo.

Machi 26, mwaka huu, Waziri Mkuu Majaliwa alipongeza NMB kwa aina mpya ya ufuturishaji wateja wao waliofunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, wadau na viongozi wa serikali, inayoenda sambamba na utoaji misaada kwa watoto watima na wanaoishi kwenye mazingira magumu na kutaka kuwapo mpango mkakati uliobeba maono hayo.

Utaratibu huo mpya wa ufuturishaji, ulianzia visiwani Zanzibar, ambako NMB ilikabidhi misaada ya vyakula, mafuta ya kupikia, sukari, sabuni na vifaa vingine kwa vituo vya Kidundo na Mazizini Orphanage, kisha kuendelea ilipofuturisha jijini Dar es Salaam, ilikovisaidia vituo vya Umrah, Tanzania Kwanza na Al Zam.

Akizungumza wakati wa Iftar iliyojumuisha viongozi wa serikali, wabunge, wateja, wadau na watoto yatima wa vituo vya Zam Zam na Darul Maarifu vya jijini Dodoma, Spika Tulia ambaye ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, alisema NMB imefanya ibada kubwa kushika mkono watoto hao katika kipindi cha Ramadhan.

"Niwapongezea kwa sadaka hii, ambayo mmenitaka mimi kukabidhi watoto hawa. Ofisa Mkuu wa Fedha ameeleza hapa maeneo mbalimbali mlikopita kufuturisha na kusaidia jamii ya wenye uhitaji, viongozi wa serikali na wateja wenu, tunawapongeza kwa sababu mmeenda kuwafuturisha wapigakura wetu huko.

"Tunathamini sadaka hii, tunapongeza NMB kwa kazi nzuri, na hii ni kwa niaba ya wote waliofuturu hapa na ambao hawawezi kupata fursa ya kuongea. Ninaomba mfahamu tu kuwa tunaheshimu sana sadaka hii mliyoitoa leo hapa na kule kote mlikofuturisha.

"Tunawashukuru sana NMB, kwa kweli mnafanya vizuri na tunawapongeza sana sana, kwa kuwa hii ni taasisi ya kifedha, inayofanya kazi za maendeleo. Tunawapongeza kwa mchango mkubwa wa maendeleo ya taifa mnaotoa kwa serikali," alisema Spika Tulia.

Akinukuu Qurani Tukufu Surah ya 99 (Az Zalzalah), aya ya saba hadi ya nane – (inayosema; Basi yule mwenye kutenda wema mdogo mfano wa mdudu chungu, atalipwa na mwenye kutenda uovu/ubaya mdogo mfano wa sisimizi, atalipwa), Spika Tulia alitabiria mafanikio makubwa NMB kwa ukubwa wa ibada za kijamii inazofanya.

"Ni matumaini yetu kuwa kwa kazi nzuri mnayofanya, ikiwamo kujali na kuthamini haya makundi maalum, mafanikio yenu yatakuwa makubwa zaidi na miaka ijayo tutashuhudia hafla hizi majimboni ama mikoani, kwa sababu Allah atakuongezeeni mafanikio kutokana na ibada zenu za kuwajali watoto hawa," alisema.

Awali Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, ambaye aliwakilisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, alisema ufuturisha wateja, waumini na wadau wao umekuwa wa muda mrefu, lakini mtazamo chanya kwa jamii ukawasukuma kufikiria kufanya kitu kwa makundi ya wenye uhitaji.

"Kila mwaka huwa tunafanya hafla hizi, lengo likiwa kudumisha ukaribu na kustawisha uhusiano mwema na jamii inayotuunga mkono, lakini namna ya kipekee mwaka huu tumekuwa tukialika watoto kutoka katika vituo vya wenye mahitaji maalum na kuwasaidia, leo tukiwa na takribani watoto 100 kutoka vituo vya hapa Dodoma," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alishukuru Spika Tulia kwa kuhudhuria hafla hiyo, akisema: "Ukiachana na ukweli kwamba hii ni ibada, lakini kwanini tunakutana? Kitabu Kitukufu cha Qurani kinatuasa na kutuhimiza umuhimu wa kukutana na kukumbushana, kwani inaaminika kwamba katika kukumbushana, ndiko tunakoweza kujengana vizuri kabisa. Kwa hiyo kusanyiko hili ni la Mungu na lina baraka zote."



# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**OBITER DEBT COLLECTION AND AUCTIONEER COMPANY LTD, MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD na MUDU COMPANY LIMITE**D kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (T) LTD**, tutauza kwa minada ya hadhara nyumba/dhamana zifuatazo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe/siku ya tangazo hili. Nyumba/Viwanja hivi zimewekwa rehani kudhamini mikopo iliyotolewa na benki ya ICBTL kwa wakopaji wafuatao.

Pia, Tangazo hili la minada ya hadhara, ni notisi ya siku kumi na nne(14) kwa wakopaji /Wamiliki /wadhamini wa mikopo hii kuhusu mauzo ya dhamana zifuatayo kwa minada ya hadhara.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ZITAKAZOUZWA**

| NO | JINA LA MKOPAJI/MDHAMINI | TAARIFA ZA DHAMANA | TAREHE YA MNADA | DALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MAFIGOLO GENERAL SUPPLIES (Mkopaji)<br>NAETWE GODFREY MLELE (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 55178 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 101460, iliyopo kiwanja na. 2004 ,kitalu'C', MBEZI LUGURUNI,MANISPAA YA UBUNGO,DAR ES SALAAM | 30/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION &AUCTINEERS COMPANY LIMITED TEL NO: 0713751800 |
| 2 | AGNES GABRIEL NTUNGUKA (Mkopaji)<br>ABUBAKAR MUSSA BAGAYA (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 5894 Dar Es salaam | Kiwanja cha makazi chenye hati nambari: 110150, Kiwanja na. 239 Kitalu '17',BUYUNI CHANIKA,MANISPAA YA ILALA , DAR ES SALAAM | 23/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION & AUCTINEERS COMPANY LIMITED TEL NO: 0713751800 |
| 3 | CARGO STAR LIMITED (Mkopaji)<br>LEO JOSEPH MANYARA (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 10000 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 84639, iliyopo kiwanja na. 14 ,kitalu'K', UKONGA,MANISPAA YA ILALA,DAR ES SALAAM | 29/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD TEL NO: 0755506970 |
| 4 | DABENCO ENTERPRISES LIMITED (Mkopaji)<br>GODFREY AUGUSTINE MPINGE(Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 76164 Dar Es salaam | Kiwanja cha makazi chenye hati nambari: 138799, lililopo kiwanja na. 6 na 8 ,kitalu'D', NIANJEMA,MANISPAA YA BAGAMOYO,DAR ES SALAAM | 26/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | MUDU COMPANY LIMITED TEL NO: 0768672367 |
| 5 | MATESO GROUP COMPANY LIMITED (Mkopaji)<br>PETER ROWLAND LAIMOS (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 19188 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari: 110468, iliopo kiwanja na. 185 ,kitalu na 9, Ilala Buyuni area-Chanika ,DAR ES SALAAM | 24/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | ORBITER DEBT COLLECTION &AUCTINEERS COMPANY LIMITED TEL NO: 0713751800 |
| 6 | LINUS PATRIC KALANDAMWAZYE T/A SICHULA ENTERPRISES Mkopaji)<br>EVA STEPHEN MHINA (Mmiliki/Mdhamini) S.L.P 111937 Dar Es salaam | Nyumba ya makazi yenye hati nambari 84643, iliopo kiwanja na.2046 , ,kitalu' 'B', KIMARA MANISPAA YA UBUNGO ,DAR ES SALAAM | 27/04/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala iliko dhamana tajwa. | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD TEL NO: 0755506970 |
| 7 | SALOME ANDREW KOMBA T/A SALOME COMMERCIAL CENTRE (Mkopaji)<br>SALOME ANDREW KOMBA S.L.P 60161 Dar Es salaam (Mdahamini/Mmiliki) | Majengo ya makazi na biashara yenye hati nambari: 55928, Kiwanja na. 1030 , Mbezi Tangi bovu kwa komba , Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam | 03/05/2024 kuanzia saa 03:00 asubuhi Mahala: Mnada utafanyika mahala ilipo dhamana tajwa. | MUDU COMPANY LIMITED TEL NO: 0768672367 |

Wanunuzi wote wenye nia na uwezo,mnakaribishwa kuja kukagua nyumba/dhamana kwa vigezo na masharti yafuatayo:

**VIGEZO NA MASHARTI YA MNADA;**

1. Mali/Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 kutokea siku ya mnada.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa na mnada utarudiwa kwa tarehe nyingine.
4. Gharama za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji "Eviction" na nyinginezo, zitakuwa juu ya Mnunuzi.
5. Ukaguzi wa dhamana unaweza kufanywa na wanunuzi, siku yoyote kuanzia siku ya tangazo hili kati ya saa tatu asubuhi na saa kumi na moja jioni.
6. Kwa taarifa zaidi,wasiliana na kampuni husika ya uuzaji

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mafanikio CAF, Simba, Yanga ziwekeze kwa wachezaji bora

**RASMI** sasa kuwa Simba na Yanga zitasubiri tena msimu ujao ili kujaribu bahati yao Ligi ya Mabingwa Afrika kama zitaweza tena kufika hatua ya makundi na kuvuka robo fainali baada ya kushindwa kufanya hivyo msimu huu.

Yanga imeshindwa kuvuka hatua hiyo, kutokana na kuondolewa kwa mikwaju ya penalti 3-2 baada ya dakika 180 za mechi zote mbili zilizochezwa jijini Dar es Salaam, Uwanja wa Benjamin Mkapa, na Loftus Versfeld jijini Pretoria, Afrika Kusini.

Simba imekuwa sasa kama ni kawaida au utamaduni wao kuishia hatua ya robo fainali ya michuano hiyo baada ya msimu huu kuchapwa jumla ya mabao 3-0, ikifungwa nyumbani Benjamin Mkapa, Dar es Salaam bao 1-0 na mabao 2-0, Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, nchini Misri, dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Kombe hilo, Al Ahly.

Ukiangalia jinsi timu za Tanzania zilivyoingia hatua hiyo na zilivyotolewa, si kwamba ni mbaya au zimeshindwa kwenda nusu fainali kwa sababu ya ubovu wa vikosi, au bahati, hapana ni viwango.

Kwanza tunazipongeza klabu hizo na viongozi wao kwa hapo walipofika kwani wameuwakilisha vema Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, maarufu kama CECAFA na si Tanzania pekee.

Kama nia itakuwa ni kuishia hatua hiyo siku zote sawa, lakini tunaona endapo timu hizo zinataka kusonga mbele zaidi ya hatua hiyo, sasa ziongeze uwekezaji kwa kusajili wachezaji wenye uwezo zaidi ya hawa waliopo. Michuano ya hii imeonyesha kuwa wachezaji waliopo wanamudu sana kutinga hatua za makundi na pia kupambana na timu zilizopo kwenye makundi, lakini linapokuja suala la robo fainali ndiyo inakuwa mtihani kuvuka hapo.

Sisi tunaona sasa Klabu za Tanzania hususan Simba na Yanga hazina budi kuachana na maneno mengi ya propaganda kutoka kwa maofisa habari wao ambao wamekuwa wakiwaaminisha vitu vingi mashabiki na wanachama wao, ambavyo vingine havipo na ni ndoito kutokea kutokana na ubora wa vikosi vyao na badala yake wawekeze ndani ya uwanja kwa wachezaji bora wenye viwango vya ya hali ya juu ambao watakuwa wanaweza kuamua mechi kubwa za maamuzi kama hizi.

Kwa timu kama ya Yanga ukiitazama haina mapungufu mengi, badala yake inahitaji mshambuliaji katili tu, mithili ya Fiston Mayele mwenye uwezo wa kuamua mechi.

Clement Mzize alikosa bao la wazi ugenini dhidi ya Mamelodi katika mechi ambapo kwa straika wa viwango vya juu, si rahisi kukuacha na kama angefunga mchezo ulikuwa unaishia hapo na kwa mara ya kwanza katika historia Yanga ingetinga nusu fainali ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.


Nayo Simba ikiwa ugenini Cairo ilipiga pasi 521, zaidi ya wenyeji wake ambao walipiga pasi 414 na kuacha wageni wakimiliki mpira kwa asilimia 56 dhidi ya 44 za Al Ahly, wakapiga mashuti 10, wakati wenzao walipiga saba tu. Pamoja na hayo ni mawili tu yaliyolenga lango, wakati Al Ahly mashuti manne katia ya saba yalilenya lango na kupata mabao mawili. Hii inaonyesha usahihi wa timu zilizowekeza vizuri kutumia nafasi chache zinazopatikana kuzigeuza kuwa mabao kitu ambacho kwa Simba na Yanga ni tatizo.

Hivyo, tunaona kwa Simba mbali ya kutakiwa kusajili straika mawili wa daraja la juu, na si kina Jean Baleke tena na Moses Phiri, bado wanapaswa kusajili mabeki wawili wa pembeni kwani waliopo tunaona wanazidi kushuka ubora wao na hata timu zinazocheza dhidi yao zimeshawasoma kwa sababu miaka nenda rudi ni hao hao tu hawana mbadala.

Tunamini Simba inatakiwa pia kuwa beki mmoja wa kati katili, mwenye nguvu, asiye na mzaha kama alivyokuwa Joash Onyango alipokuwa kwenye kiwango cha juu, kwa sababu imekuwa ikiruhusu mabao kirahisi ambayo kwa timu kubwa kama hiyo hayatakiwi kufungwa.

Aidha, hatutarajii kuziona kila msimu zikisajili wachezaji wapya karibu zaidi ya sita kwani huko nako kunachangia kuunda kikosi cha ushindani kutokana na kuhitaji muda wa kuzoeana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba, Yanga, mkuki mtamu kwa nguruwe, lakini kwa binadamu?...

**WALA** sipepesi macho kusema timu za Simba na Yanga ndizo zinazonufaika na maamuzi mabovu ya baadhi ya waamuzi wa Tanzania kwenye Ligi Kuu ya Tanzania.

Na wala sitaki kuorodhesha matukio ya mechi mbalimbali kwa misimu kadhaa ya Ligi Kuu, ila yeyote atakayesoma anaweza kukumbuka baadhi ya mechi ambazo Simba au Yanga zikicheza na timu zingine za Ligi Kuu zimekuwa zikinufaika zaidi na makosa ya kibinadamu ya waamuzi.

Baadhi ya marefa wamekuwa wakifungiwa na wengine wakiachwa, ikitafsiriwa kuwa ni makosa tu ya kibinadamu.

Waswahili na wahenga wamekuwa na misemo mingi sana. Upo unaosema mtenda akitendewa huhisi kaonewa, mwingine ni ule unaosema, siku zote mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.

Wakiwa na maana mkuki ukipigwa nguruwe inaoenekana ni kawaida, lakini ngoja apigwe binadamu ni tafrani tupu.

Siandiki hili kwa kukataa kuwa Simba na Yanga zilinyongwa na waamuzi kwenye 'usiku wa balaa', Ijumaa iliyopita katika mechi zao zilizochezwa Misri na Afrika Kusini.

Wala haikuhitaji VAR kujua kuwa, mpira uliopigwa na Stephane Aziz Ki uligonga mwamba wa juu na kudundia ndani kwa asilimia 100, hivyo lilitakiwa liwe bao halali dhidi ya Mamelodi Sundowns kwenye Uwanja Loftus Versfeld jijini Pretoria, Afrika Kusini.

Kama lingekubaliwa, saa hizi Yanga ingekuwa hatua ya nusu fainali, ikijiandaa kucheza dhidi ya Esperance ya Tunisia, lakini ikatolewa kwa mikwaju ya penalti 3-2, baada ya kucheza mechi mbili nyumbani na ugenini bila bao lolote.

Simba ilinyongwa Cairo, mwamuzi alipopeta, Kibu Denis alipofanyiwa madhambi ndani ya eneo la hatari, ambapo ilibidi ipate penalti ambayo kama ingefunga ingeweza kubadilisha kila kitu kwenye mchezo huo.

Dakika za majeruhi, Fondoh Che Malone aligongana na mchezaji mmoja wa Al Ahly, lakini mwamuzi aliweka 'tuta' lililozaa bao la pili. Kwa tukio lilivyotokea haikustahili kuwa penalti, lakini licha ya wachezaji wa Simba kumzonga, lakini ikawa kazi bure.

Matukio haya yote kwenye mechi ya robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika, yananikumbusha baadhi ya matukio yanayotokea kwenye baadhi mechi za Ligi Kuu, ambapo timu hizi kubwa hunufaika na kupata pointi tatu au moja ambazo hazikustahili.

Nimeona mashabiki wa timu zote mbili wakilalamika sana. Wakilia sana juu ya maamuzi ya waamuzi waliochezesha mechi hizo, ikanikumbusha kuwa kumbe kila mkubwa ana mkubwa wake.

Binafsi, sipingi malalamiko yao, ila nataka sasa mashabiki wa Simba na Yanga wavae viatu vya kina Ihefu FC, KMC, Coastal Union, Geita Gold, Prisons, Mashujaa FC, Namungo, Tabora United wanavyokuwa wanalia na maamuzi ya baadhi ya waamuzi.

Wajue uchungu wanaoupata mashabiki na viongozi wa timu hizo wanavyony'ongwa wakiwa katika harakati za kusaka na wao kucheza mechi za kimataifa.

Ndiyo maana nimeona Maofisa Habari za Azam FC wakichapisha video mbalimbali fupi zinazoonyesha baadhi ya matukio ambayo hawakutendewa haki na waamuzi.

Nadhani kama viongozi wa timu zingine kimoyomoyo watakuwa wamefurahi kwani wanataabika sana, na wanapopiga kelele wao na makocha wao hakuna kingine wanachoambulia zaidi ya kibano.

Nimeandika hili kuwakumbusha mashabiki wa soka nchini kuwa linapotokea tatizo au mwamuzi amevurunda, wote wanatakiwa kusimama kwa pamoja ili kukemea na si kugawana upande. Hata mashabiki wa timu iliyonufaika wanatakiwa kukemea kitu hicho kwani leo linaweza kuwa jema kwako, lakini kesho likamkuta mwingine.

Kama ambavyo mashabiki wa Simba na Yanga wote kwa sasa wameungana kukubali kuwa wameonewa katika mechi zao za robo fainali, hivyo hivyo sasa wawe pamoja kukemea siku ambayo timu zao zinapokuwa zimeonekana kubebwa na waamuzi dhidi ya timu za Ligi Kuu.

Jambo hili litaanza kuondoa dhana kwa mashabiki wa timu hizi kuwa timu zao tu ndizo zinatakiwa kunufaika na makosa ya waamuzi na ni dhambi kwa timu zingine.

Nadhani hii itaanza kuwa mfano, na kutengeneza mazingira mazuri ya kupambana hata na uonevu kwenye mechi za kimataifa.

HABARI KITAIFA

# Zaidi wananchi 11,000 wapatiwa tiba moyo


**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kupitia tiba inayojulikana kama Dk. Samia Suluhu Hassan Outreach Services, imefika mikoa 13 na kutoa huduma ya moyo kwa wananchi 11,254.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Anna Nkinda, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumzia tuzo mbili za heshima za uhusiano na mawasiliano katika kutoa elimu kwa umma kuhusu magonjwa ya moyo na kutoa huduma kwa jamii ya upimaji na matibabu ya magonjwa ya moyo ambazo JKCI ilipata.

Tuzo hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Chama cha Maafisa Uhusiano na Mawasiliano Tanzania (PRST), mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi.

Nkinda alisema kwenye taarifa yake kuwa JKCI imeshinda tuzo hizo kupitia huduma za tiba mkoba zinazojulikana kwa jina la Dk. Samia Suluhu Hassan Outreach Services inazozifanya kwa kufanya upimaji na matibabu ya magonjwa ya moyo kwa kuwafuata wananchi mahali walipo.



Alisema upimaji huo unakwenda pamoja na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakiwemo ya moyo na matumizi sahihi ya dawa za moyo, kuwajengea uwezo wataalamu wa afya wa jinsi ya kuwatambua wagonjwa wa moyo na kufanya utafiti wa magonjwa ya moyo.

Alisema ushindi huo pia umetokana na mchango mkubwa unaotolewa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano katika kuuhabarisha umma kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi pamoja na kutoa elimu ya magonjwa ya moyo kwa wananchi.

Wakati huo huo, Nkinda alisema wataalamu wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Iringa wanatarajia kuendesha kambi ya siku tano kupima maradhi ya moyo kupitia huduma ijulikanayo kama Dk. Samia Suluhu Hassan Outreach Services.

Nkinda alisema upimaji huo utafanyika kwa watoto na watu wazima kuanzia Aprili 15 hadi 19 na pia kutakuwa na wataalamu wa lishe ambao watatoa elimu ya lishe bora ambayo itawapa wananchi uelewa na kufuata mtindo bora wa maisha.

Alisema mtindo bora wa maisha utawasaidia wananchi kuondokana na magonjwa ya moyo ambayo ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza yanayoweza kuepukika iwapo watafuata ushauri wa wataalamu wa afya.

Nkinda alisema wananchi watakaogundulika kuwa na matatizo ya moyo watafanyiwa uchunguzi zaidi na kupatiwa matibabu hapo hapo na wengine watapatiwa rufaa kwenda kutibiwa JKCI jijini Dar es Salaam.

"JKCI inawaomba wananchi watumie fursa hii kujitokeza kwa wingi kupima ili kujua kama wana matatizo ya moyo na wale watakaogundulika waweze kutibiwa mapema kabla hali haijawa mbaya," alisema.



Naibu Mkurugenzi wa Fedha, Halotel Tanzania, Najib Ferej (watatu kushoto) akiwa na baadhi ya viongozi wa Mtaa wa Bwawani na mashekhe wakati wa iftar iliyoandaliwa na kampuni hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAMPICHA WETU**

# Halotel yaiweka pamoja jamii mfungo wa Ramadhan

**Na Zuwena Shame**

KAMPUNI ya Halotel Tanzania imefuturisha wakazi wa Makumbusho na wafanyabiashara wadogo kwa lengo la kuileta pamoja jamii katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Iftar hiyo iliwakusanya wafanyabiashara wadogo wa soko la makumbusho katika mtaa wa Bwawani, Manispaa ya Kinondoni.

Akiongea wakati wa ghafla hiyo, Naibu mkurugenzi wa fedha wa Halotel, Najib Ferej alisema kampuni hiyo inaamini katika umoja na mshikamano kama kaulimbiu yao inavyosema 'Pamoja kwa Ubora' na imeona ni muhimu kusaidia juhudi za serikali kuleta watu pamoja na kukuza uhusiano mzuri wa jamii inazowazunguka.

"Katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, Halotel kwa ushirikiano na serikali tunajivunia kuandaa iftar kwa ajili ya jamii yetu. Hii ni ishara ya Umoja wetu, mshikamano na undugu unaotuunganisha sote. Ni wakati wa kushiriki, kusadiana na kuimarisha mahusiano yetu katika jamii," alisema Ferej.

Pia kupitia udhamini huo, Halotel iliwezesha uongozi wa mtaa wa Makumbusho kufanya tukio hilo kuwa la kipekee na la kumbukumbu kwa wakazi wa mtaa huo kwa kuwa inatambua umuhimu wa kujenga jumuiya zenye upendo na kuwa tukio hilo litakuwa fursa nzuri ya kuimarisha mahusiano ya kijamii na kukuza utamaduni.

Naye, mwenyekiti wa serikali za mitaa wa Bwawani, Ismail Mwenda alishukuru kampuni ya Halotel Tanzania kuonesha nia ya kuunganisha watu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani.

"Hii ni chachu katika jamii kampuni inapoamua kuunganisha watu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, inaonesha upendo na mshikamano kati ya watu wa Makumbusho na jamii kiujumla" alisema Mwenda.


MWAMBA GENERAL AUCTIONEER & COURT BROKER CO.

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

EXAUD JOACHIM HUGHO .......MDAI

DHIDI YA

SEIF ALLY KULUNGE ......MDAIWA.

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA NOESIS ATTORNEYS (MAWAKILI) KUPITIA MTEJA WAO NDUGU EXAUD JOACHIM HUGHO TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MASHINE ZA KUPRINT AINA YA **XEROX CORPORATION PRODUCT IDENTIFIER F38-1VOLTS/TRANSACTION 208-240V AMPS /AMPERAGE 12A / HERTZ / FREQUENCY 50/60/ HS.** ZILIZOPO MKOA WA DODOMA WILAYA YA CHAMWINO MTAA WA MNADANI SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 20/4/2024 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA, MNADA UTAFANYIKA MAHALA DHAMANA ZILIPO.

Mnunuzi utatakiwa kulipia asilimia ishirini na tano (25%) ya bei ya mnada itakayofikia papo hapo na Na asilimia (75%) ilipwe ndani ya siku kumi nne (14)

Wote Mnakaribishwa
MAWASILIANO:-
0655 112841/ 0688 443302.



**NOTICE OF APPEAL TO BENEDICTO R. IJUMBA, 2ND RESPONDENT**

**IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT DARE ES SALAAM.**
**CIVIL APPEAL NO. ...... OF 202...**
**IN THE MATTER OF AN INTENDED CIVIL APPEAL**

**BETWEEN**

**VICTORIA RWEIKIZA —APPELLANT**

**VERSUS**

1. **ALEX MSAMA MWITA —1ST RESPONDENT**
2. **BENEDICTO R. IJUMBA — 2ND RESPONDENT**
3. **NOELA O. ISHEBABI—3RD RESPONDENT**

*(Appeal from the decision of the High Court of Tanzania (Land Division) at Dar es Salaam (Madam Justice Msafiri J.) dated 19th September, 2022 in Land Revision Number 08 of 2022, being a decision)*

## NOTICE OF APPEAL

***(Under Rule 83 of the Tanzania Court of Appeal Rules, 2009)***

**TAKE NOTICE that VICTORIA RWEIKIZA,** being dissatisfied with the decision of Honorable Madam Justice Msafiri, J given at Dar es Salaam at around 11am on the 19th day of September, 2022, intends to appeal to the Court of Appeal of Tanzania against the whole of the said decision.

The name and address of the Appellant is:
VICTORIA RWEIKIZA
P.O.BOX 25484,
DAR ES SALAAM, TANZANIA
MOB: +255 745 007 200

The name and address of the Appellant's advocate is:

AUDAX KAHENDAGUZA VEDASTO (ADVOCATE),
ADARE ADVOCATES
BOOK HOUSE,
BOX 77586, DAR ES SALAAM
TEL. 0754/0788 594 294.

The name and address of the Respondents are:

ALEX MSAMA MWITA, DAR ES SALAAM —1st Respondent
&
BENEDICTO R. IJUMBA
BOX 22601, DAR ES SALAAM — 2ND RESPONDENT
&
NOELA O. ISHEBABI
BOX 25484, DAR ES SALAAM —3RD RESPONDENT

It is intended to serve this Notice on:

1. MRINDOKO LAW CHAMBER,
PLOT NO. 183, BLOCK 11,
UNDALI STREET-UPANGA
BOX 14277, DAR ES SALAAM
MOB: 0715 452 572 —FOR THE 1st RESPONDENT
&
2. BENEDICTO R. IJUMBA
BOX 22601, DAR ES SALAAM — THE 2ND RESPONDENT
&
3. OBED KASAMBALA ADVOCATE
2ND FLOOR, MAVUBO HOUSE
DAR ES SALAAM —FOR THE 3RD RESPONDENT

Dated at Dar es Salaam this **5th** day of **October, 2022**

Signed
AUDAX KAHENDAGUZA VEDASTO
ADVOCATE FOR THE APPELLANT

To: The Registrar of the High Court of Tanzania (Land Division) at Dar Es Salaam

Lodged in the High Court of Tanzania (Land Division) at Dar Es Salaam this 11 of October 2022

REGISTRAR

DRAWN AND LODGED BY
AUDAX KAHENDAGUZA VEDASTO (ADVOCATE),
ADARE ADVOCATES (formerly AUDA & COMPANY ADVOCATES)
BOOK HOUSE, MWINYIJUMA ROAD
(OPPOSITE MAKUMBUSHO DISPENSARY SIGN BOARD)
MTAA SINDANO, MAKUMBUSHO WARD,
KINONDONI, DAR ES SALAAM.
P.O. BOX 77586, DAR ES SALAAM
E-mail: auda@audaadvocates.com/advdkd@yahoo.com
TEL. 0754/0788 594 294

# Fisi wazua taharuki katika uwanja wa ndege Mtwara

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

FISI wamezua taharuki mkoani hapa kwa watendaji na kuharibu miundombinu ya uwanja wa ndege ikiwamo kutafuna nyaya za taa na mitambo.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki kuhusu tukio hilo, Kaimu Meneja wa uwanja huo, Shadrack Mabula, alisema fisi hao wamekuwa tishio katika uendeshaji wa shughuli zao.

Alisema kiwanja kinafanya shughuli zake saa 24 na endapo ndege itatua usiku kukawa na fisi inaweza kuhatarisha usalama wa wafanyakazi na abiria na sasa wamelazimika kuanzisha msako wa haraka kwa ajili ya kuwakamata wanyama hao.

Ofisa Wanyamapori mkongwe katika tasnia hiyo ya wanyamapori, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Richard Milanzi alisema; "tumejitahidi muda wa siku mbili ikawa tunashinda nao, tulichokifanya tukasema hapa cha msingi tutafute chambo maana mara nyingi fisi anapenda sana mzoga tuweke kwenye mazingira ambayo anapita pita."

"Tukapata chambo tukaweka pale mazingira ambayo wanapitapita sisi wenyewe tukajificha, majira ya saa tatu hivi usiku wakaja wawili akapigwa mmoja akaanguka mmoja akakimbia, tukaendelea kujificha kama dakika 20 akaja mwingine akapigwa baada ya hapo tumekaa mpaka saa sita usiku tukasema sidhani kama watakuja wengine basi tukaenda kupumzika," alisema Milanzi. Aidha, alisema fisi waliyouawa wote hawana mikia huku Ofisa Wanyamapori katika halmashauri hiyo, Rajabu Ndete akilezea mazingira yanavyokuwa wakati wanapowaua wanyama hao.

"Unapopiga fisi usiku au mnyama yoyote yule ukishajua ameanguka wewe unaenda kupumzika au kwenda kufanya kazi sehemu nyingine kufanya msako sasa ukirudi huku chochote kinaweza kutokea."

Mkongwe katika Tasnia hiyo ya wanyamapori (Milanzi) alisema suala la fisi kutokuwa na mikia ni kawaida mnyama anapopigwa hawezi kuachwa kama alivyo, lazima atolewe kipande fulani na kila wakati fisi anapopigwa lazima atolewe mkia.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, akizungumza na watumishi, wadau mbalimbali baada ya Iftar iliyoandaliwa na mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## TANAPA yaishauri h'shauri Ngara fursa kupata fedha

**Na Judith Julius,** NGARA

MAMLAKA ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), imeishauri Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kutenga eneo kwaajili ya hifadhi ili kujipatia fedha zitakazotumika kwa maendeleo ya wilaya.

Ushauri huo ulitolewa katika mkutano wa kujadili utekelezaji wa milki za ardhi uliofanywa na halmashauri wilayani humo, mwishoni mwa wiki.

Kaulimbiu ya mkutano huo 'Usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi kwa ustawi wa jamii', ikilenga zaidi migogoro ya wakulima, wafugaji na TANAPA.

TANAPA ilisema ipo haja kwa Wilaya ya Ngara kutengeneza hifadhi ili kujikwamua kiuchumi kutokana na kuwa na wageni wanaotoka nchi jirani za Rwanda na Burundi.

Ilisema kupitia hifadhi hiyo, Wilaya ya Ngara inaweza kunufaika kwakupata fedha za kigeni kusaidia kukuza zaidi maendeleo yake.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wilayani humo, Chrispine Medard Kamugisha, alitaja baadhi ya maeneo yenye migogoro ya ardhi kuwa ni Rusumo na Mshikamano, akibainisha kuwa maeneo yote hayo yamepakana na nchi ya Rwanda.

Mwenyekiti wa wafugaji, Alex Nyamkala, alisema changamoto wanazokutana nazo katika shughuli zao za ufugaji ni maeneo finyu ya kulishia mifugo yao.

Alishauri serikali wilayani Ngara kuweka viashiria au alama zinazoonyesha eneo la Hifadhi ya Taifa ili majirani , Rwanda na Burundi, wanapovuka mipaka hiyo kuingia nchini Tanzania waweze kuzitambua.

Ofisa wa Hifadhi, Enock Mponzi, aliahidi ya kuyafanyia kazi maombi yanayohusu hifadhi hiyo.

# MSD yaja mpango wa pamoja ununuzi vifaa tiba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na adha ya kuchelewa kupokea bidhaa za afya hasa vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Bohari ya Dawa (MSD) imekuja na mpango wa pamoja wa ununuzi wa mwaka mzima kati yao na mteja ili kuwa na maoteo na mipango sahihi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye mkutano wa wateja na wadau wa MSD Kanda ya Dodoma, Mkurugenzi Mkuu MSD, Mavere Tukai alisema;

"Kifaa tiba ukiagiza wastani inachukua miezi saba hadi tisa kupata, vifaa tiba vingi havikai kumsubiri mteja vinasubiri oda ndio vitengenezwe, lazima mzalishaji ataomba muda wa kuzalisha ndio asafirishe."

Alisema kifaa kinapowasili nchini kinapitia michakato mbalimbali ikiwamo kuangalia ubora.

"Sasa haya mambo kama hatujashirikiana na wateja kuwaambia kifaa kiagizwe mapema, kila siku utakuwa na changamoto ya kuchelewa kupata kwa hiyo tunatengeneza uelewa wa pamoja na mbinu mbadala za kufanya mauzo na manunuzi," alisema.

Alisema lengo la kufanya mageuzi hayo ni kuifanya MSD kuwa na muundo wa kisasa na kutoka kwenye muundo wa kiutawala na kuwa wa kiutendaji.

"Tunaangalia namna ya kushirikiana na benki, tusisubiri tu serikali itupe, kakope mkopo wa riba nafuu umnunulie mteja bidhaa yake ili akipata akulipe, badala ya kusubiri serikali kifaa kikichelewa unaanza kulia tunatoka huko," alisema.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwaagiza wadau wa afya nchini, kufanya maoteo ya bidhaa za afya kwa usahihi na kwa wakati ili kusaidia MSD kuwa na takwimu sahihi ili kuagiza kwa wazalishaji na washitiri.

Senyamule alisema ni lazima katika ununuzi wa vifaa, upangaji bajeti wadau hao washirikiane na MSD ili kuondokana na kero zinazojitokeza.

"Kila mtu ana jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya bidhaa za afya ili kuleta tija kwa wananchi kwa kutekeleza haya wananchi watapata huduma bora katika vituo vya kutolea huduma za afya bila manung'uniko," alisema.



## Bil.48/- zatengwa uboreshaji miundombinu elimu IAA

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya Sh. bilioni 48 zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Mratibu Msaidizi wa HEET, Emmanuel Palangyo, alieleza hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha kwanza cha Kamati Maalumu ya Ushauri ya Kisekta IAA.

Alisema kuwa mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2021 na taasisi 22, vikiwamo vyuo 19 na taasisi tatu, ambazo zinasimamia elimu, utekelezaji wake utafikia ukomo mwaka 2026.

Alisema katika mradi huo, IAA imepatiwa Dola za Marekani milioni 19, sawa na Sh.bilioni 48 na kiasi hicho cha fedha kitatumika kwenye maeneo saba ya utekelezaji wa mradi.

"Eneo la kwanza itakuwa ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ambapo tutakuwa na ujenzi katika kampasi tatu za Arusha, Babati na Songea, pia eneo la pili ni kuuhisha mitaala na ufundishaji unaokwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia.

"Eneo la tatu ni matumizi ya TEHEMA katika ufundishaji, nne ni kuangalia namna taasisi hiyo, itakavyoweza kujiendesha kutokana na mapato mengine pasipo kutekemea ada za wanafunzi.

"Pia eneo la tano wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo kuwaunganisha na mtandoa wa ajira na kujiajiri wenye kutokana na mafunzo waliyopata, sita kuwajenge uwezo watumishi hasa walimu ili waweze kuongeza ufanisi katika ufundishaji na eneo la mwisho ni usimamizi wa mradi kwa ujumla," alisema Palangyo.

Naibu Mkuu wa Chuo cha IAA, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam, Prof. Epaphra Manamba, alisema katika kikao hicho wamejadiliana namna chuo kinavyoweza kukua pamoja na kufanya ulinganisho wa wahitimu wanaotoka hapo na mahitaji ya soko la ajira.

"Kumekuwapo na mijadala mingi kutoka kwa wadau wa elimu wakiwamo waajiri kuwa wahitimu wengi hawana ujuzi kutosha wa kutekeleza majukumu yao kwa vitendo wanapokwenda kazini ambapo wamekuwa wakiwaangalia watu ambao wanakwenda sambamba na mahitaji ya soko.

"Kwa kuzingatia hilo IAA, tuliona tuandae kamati maalum ambayo inatakuwa na jukumu la kutoa ushauri ambapo wajumbe wametoka kwenye mbalimbali ikiwamo sekta za umma na binafsi ambazo ni wabobezi katika masuala ya ajira na mahitaji ya soko na watakuwa na kazi ya kuangalia mitaala yetu ya elimu iendane na soko la ajira na mahitaji ya jamii na namna ya kuwafundisha wanafunzi na kutumia mitaala hiyo," alisema Prof.Manamba.

Alisema kamati hiyo itakuwa na kazi ya kupitia programu zao na kuangalia zile ambazo zinahitajika kufanyiwa marekebisho na zinazofaa kuendelea kutumika ili mwanafunzi anapotoka chuoni hapo aweze kunufaika mwenyewe na taifa kwa ujumla kwa kuwa jamii inahitaji wataamu mbalimbali.

Kadhalika, Mratibu wa Kamati Maalumu ya Ushauri wa Kisekta IAA, Lona Boniface, alisema kamati hiyo itakuwa muhimu kwa chuo hicho, kwa kuwa itawasaidia kuungalisha mitaala yao pamoja kuwawezesha wanafunzi kuunganishwa na fursa mbalimbali.

# Usaili waombaji wa ajira serikalini sasa ni kidijitali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SERIKALI imezindua mfumo wa kidijitali wa kufanya usaili wa waombaji wa ajira, lengo likiwa ni kupunguza usumbufu usio wa lazima wa waombaji kusafiri usiku na mchana.

Mfumo huo utakaofanya kazi katika vituo 32 vya Tanzania Bara na Zanzibar sasa utawafuata wasailiwa waliko huko wilayani na mikoani.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, akizindua mfumo huo mwishoni mwa wiki katika Wilaya ya Babati, alisema Tanzania Bara itakuwa na vituo 30 na Zanzibar itakuwa na viwili katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Alisema baada ya kuzindua mfumo huo, utaanza kwa kufanya kazi ya kusaili nafasi 23 za maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambapo tayari kuna waombaji 2,325 ambao wote wangelazimika kusafiri kwenda Dodoma kufanya mtihani wa usahili.

Waziri huyo, alisema mfumo huo hautawaumiza watu tena kutumia gharama nyingi kusafiri.

Aidha, alisema mfumo huo wameukubali baada ya kupokea maoni na ushauri wa wabunge na wadau ambao waliomba serikali kuanzisha ili kuondoa usumbufu kwa waombaji wa ajira.

"Tangu sekritalieti ya ajira ianze kazi kumekuwa na mafanikio hii inaondoa upendeleo uliokuwa unafanywa na baadhi ya taasisi,"alisema.

Vilevile, alisema watakaosahiliwa kwenye nafasi hizo 23 na wakafanya vizuri ila baadhi wakabaki kutokana na uhitaji mdogo, wengine watawekwa kwenye kanzi data, ili ikitokea nafasi za namna hiyo tena wanachukuliwa waliokuwa wamefanya vizuri.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Sekritalieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Innocent Boman, alisema mfumo huo wa kidigitali utakuwa endelevu na usahili utakuwa unafanyika kwa pamoja vituo vyote nchi nzima.

Kwa mujibu wa Boman, wanajipanga vizuri kuusimamia mfumo huo ili kuwapunguzia adha waombaji wa ajira.

Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA Manyara, ambacho ni miongoni mwa vituo vya usaili nchini, Nansanga Massangya, alisema mfumo huo utawasaidia watu ambao hawana uwezo na uzuri ni mfumo rafiki.



Watuhumiwa nane kutoka kijiji cha Kambai, kata ya Kwezitu, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wanaotuhumiwa kuchoma moto gari aina ya Suzuki la Ofisa kilimo wa kata ya Tongwe, Subira Mmbago, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya wilaya hiyo, mwishoni mwa wiki, kusomewa mashtaka yanayowakabili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Bashungwa atishia kumnyima ajira mkandarasi barabara

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ametishia kuzuia Kampuni ya M/S Jiangxi Geo Engineering Group Ltd, kupewa zabuni nyingine ya ujenzi wa barabara za lami nchini, iwapo mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mbulu/Garbabi, na Haydom/Labay utaendelea kusuasua.

Badala yake, amemtaka mkandarasi huyo kufanya kazi usiku na mchana ili kumaliza mradi wa kilomita 57 kwa wakati.

Bashungwa alitishia kuizuia kampuni hiyo, mwishoni mwa wiki, wakati wa mkutano wake wa hadhara katika Kata ya Dareda na Kata za jirani za Wilaya ya Babati, muda mfupi baada ya kushuhudia utiaji sahihi mkataba wa ujenzi wa barabara kilomita saba, kwa kiwango cha lami kati ya Dareda/ Dareda Misheni.

Alisema mkandarasi huyo, alipewa kazi ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami ya kilomita 25 kutoka Mbulu/Garbabi na kilomita 25 Haydom/ Labay, na sasa ameongezewa kilomita saba kutoka Dareda hadi Dareda Misheni.

"Mkandarasi nataka ukipata fedha ufanye kazi usiku na mchana, nitaenda kukuombea fedha kwa Rais (Samia) unazodai za Mbulu/Garbabi. Sitaki kusikia visingizio tena,"alisema Bashungwa

Aidha, alisema mkandarasi huyo ameongezewa kilometa saba hivyo anataka kazi iende haraka na uzuri ni mkandarasi wa kimataifa ana uzoefu.

"Hizi kilomita saba ni kama uji tu kwa kuwa unazo kilometa nyingine 50 mkoa huu ukifanya vizuri hizi kilometa 57, utakuwa na faida ukichemka hupati kitu tena mkoa huu,"alieleza

Bashungwa, alisema licha ya kazi hizo Rais alitoa maelekezo kwa wizara hiyo kuwa waboreshe miundombinu ya Wilaya ya Hanan'g ambao walipata maafa ambapo alitaja vitu vitakavyoboreshwa kuwa ni kujenga tabaka la juu la lami kilometa mbili.


Maelekezo mengine ni kufunga taa za barabarani, kujenga mitaro, malarvati sita kujengwa na kuweka vivuko vya watembea kwa miguu.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mohamed Besta, alisema ujenzi wa barabara hiyo ya Dareda kati hadi Dareda Misheni, utagharimu Sh. bilioni 9.8.

Mtendaji mkuu huyo alisema ujenzi wa barabara hiyo utasimamiwa na wataalamu wa ndani.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema barabara hiyo itaongeza thamani ya mazao ya wananchi na wakulima hawatapangiwa bei na madalali bali wao ndio watawapangia bei madalali.

Sendiga alimuomba waziri kuutengea mkoa huo bajeti ya kimkakati ili iweze kusaidia kipindi cha mvua kwa kuwa mvua ikinyesha hamna fedha zinasubiri madhara yakitokea.





# RC Mtanda aahidi kuanzia alipoishia Amos Makalla

**Na Zatifa Ramadhan,** SAUT

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda ameahidi kuyafanyia kazi mambo yote aliyoasisi mtangulizi wake, Amos Makalla na kuhakikisha atatoa ushirikiano kwa watumishi wote.

Aliyasema hayo juzi wakati wa makabidhiano ya ofisi na alikuwa Mkuu wa Mkoa huo na sasa ameteuliwa kuwa Katibu wa Itikadi Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla.

Alisema katika uongozi wake anaamini zaidi katika ushirikiano, hivyo anategemea kutoka kwa wote katika ofisi hiyo watampa ushirikiano.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makalla alimtaka Mtanda kusimamia ipasavyo miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa mkoani hapa.

"Nimerudi kwenye kazi ninayoipenda sana au ninaweza kusema upele umepata mkunaji, sisi ni kama wanajeshi unavaa gwanda unaingia vitani, hivyo nakusisitiza kusimamia utekelezaji wa miradi yote ya kimkakati katika mkoa huu," alisema na kuongeza:

"Naamini utakuwa mwepesi wa kuzunguka kujua matatizo ya wananchi na kuyatatua," alisema.

Makalla alisema kati ya kazi ngumu alizokutana nazo tangu anateuliwa kuingia mkoani hapa ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege Mwanza ambapo kila mtu hakutaka kuliona kama lilivyokuwa, hivyo kupokea ujumbe nyingi zikita ufanyiwe kazi.

"Kutokana na kuwa pia yalikuwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ilikuwa ni kazi yangu ya kwanza nikawabadilishia wasimamizi kutoka Ofisi ya Mkoa kurudi Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na sasa ujenzi wake umeanza. simamia ili uwe uwanja wa kimataifa," alisema Makalla.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Mwaka wa Fedha 2021/22 uwanja huo ulijengwa chini ya viwango, huku vifaa vya ujenzi vya Sh. milioni 233 vikitelekezwa katika eneo la ujenzi.

Vifaa hivyo ni pamoja na vigae vya sakafu, ubao wa saruji na nyuzi, mabati, nondo, saruji, vigae vya ukutani, rangi ya mafuta na rangi ya nje vyenye thamani ya Sh. milioni 233.46.




Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara Benki ya Azania, Dk. Rhimo Nyansaho (katikati) akikabidhi magodoro 100 kati ya 200 yenye thamani ya Sh. milioni nane kwa Mkuu wa Gereza la Mugumu, wilayani Serengeti mkoani Mara, Michael Mafwele yaliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya wafungwa na mahabusu katika gereza hilo na Gereza la Tabora B, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu Msaidizi wa gereza la Tabora B, Albert Beda na maofisa wa magereza hayo, Lucas Muhindi (kulia) na Christopher Maningu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge afuturisha waumini misikiti 113

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MBUNGE wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza, ametoa chakula kwa ajili ya futari kwa waumini wa dini ya kiislamu katika misikiti 113 Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera.

Chakula hicho kilikabidhiwa mwishoni mwa wiki na msaidizi wake, Jasson Lwankomezi, kwa Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA) Wilaya ya Bukoba, Ahmed Baitu, ambaye alipokea kwa niaba ya misikiti yote ya wilaya hiyo.

Akizungumza kwenye makabidhiano hayo, Lwankomezi, alisema imekuwa kawaida kwa mbunge huyo kutoa chakula cha futari kila unapofika mwezi wa Ramadhani.

"Tunaomba mpokeee futari kutoka kwa Dk. Rweikiza ambayo ameitoa kwa waumini wote wa jimbo hili kwa heshima kubwa naomba niwakabidhi na tutasafirisha mpaka kufika kwenye maeneo husika," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea chakula hicho, Katibu wa BAKWATA, Baitu alisema waislamu wamepokea kwa mikono miwili sadaka hiyo.

Hivyo, alitoa shukrani kwa mbunge huyo kwa msaada huo ambao umekuja wakati mwafaka wakati huu wa mfungo wa mwezi wa Ramadhani.

"Kwa dhati kabisa kwa niaba ya wilaya yetu tunamshukuru sana mbunge na tunamwomba Mungu amwongezee zaidi kwa wema huu aliouonyesha kwetu, tunamwomba Mungu amwongezee alipotoa na aendelee kumwongezea pale alipotoa," alisema Katibu wa BAKWATA.

Imamu wa Msikiti wa Katoma, Yakub Abdalah, alisema msaada huo unaonyesha namna mbunge huyo anavyojali imani za wengine na kuiomba jamii kuishi kwa upendo wa namna hiyo.

Alisema mtu anaweza kuwa na mali lakini asiwe na mapenzi na wenzake, lakini hali hiyo ni tofauti na Dk. Rweikiza ambaye amejaliwa upendo wa dhati kwao pia kila mwezi wa Ramadhani amekuwa akitoa msaada kama huo na kazi yao ni kumwombea dua.

Mwenyekiti wa Vijana BAKWATA Wilaya ya Bukoba Vijijini, Shaf Abdulkadiri, alisema msaada huo ambao Dk. Rweikiza amekuwa akiutoa mara kwa mara unaonyesha upendo alionao kwa watu wenye imani nyingine na kuomba jamii kuiga mfano huo.

Alisema: "Kwa niaba ya vijana wa jimbo hili napenda kumpongeza na kumshukuru mbunge wetu kwa kweli amefanya kitu kikubwa sana na cha kuigwa na jamii nzima tunamwomba Mungu amzidishie na aendelee kumwongezea pale alipotoa".

## Mtatiro aanza kwa kulivunja Baraza la Usuluhishi la Kata

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro amemuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, kulivunja Baraza la Usuluhishi la Kata ya Ndembezi, kutokana na kushindwa kushughulikia utatuzi wa kero za wananchi.

Alitoa maagizo hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema wananchi wa kata hiyo wana kero nyingi ambazo zingine zipo chini ya uongozi wa kata likiwamo baraza hilo lakini hazitatuliwi.

Hivyo alimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga kulivunja baraza hilo mara moja na kuunda lingine ambalo litashughulikia matatizo ya wananchi.

"Mikutano yangu yote ya kusikiliza kero za wananchi katika kata zote za Manispaa ya Shinyanga, hapa ndipo nimekumbana na kero nyingi harafu eti kuna Baraza la Usuluhishi la Kata, na kuagiza Mkurugenzi hadi kufikia Jumatatu uwe umeshalivunja baraza hili," alisema Mtatiro.

Alisema kuna baadhi ya kero za wananchi ambazo zingine ni za kushughulikiwa na viongozi likiwamo na baraza la usuluhishi, lakini hazitatuliwi hadi kusubili viongozi wa juu, huku wananchi wakiwa na kesi nyingi mahakamani ambazo utatuzi wake ni ngazi ya chini, kuwataka viongozi kila mmoja atekeleze wajibu wake.

Aidha, aliwaagiza maofisa wa Biashara wa Manispaa ya Shinyanga kuacha tabia ya kufunga biashara za wananchi yakiwamo maduka ambao wamekuwa wakiwadai ko.

Bali aliwaagiza watumie busara na siyo nguvu, ikiwamo kuandikishana mikataba ya kulipa taratibu hadi kumaliza deni.

Pia, aliwaagiza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), kuhakikisha wanazifungua barabara za mitaa katika kata hiyo ya Ndembezi ambayo haina barabara kabisa.

Mtatiro pia aliitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka huduma ya umeme kwenye maeneo ambayo hayana umeme katika Kata ya Ndembezi.

Baadhi ya wananchi wa eneo hilo wakiwasilisha kero zao kwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, walilalamikia suala la ukosefu wa barabara, huduma ya umeme, kukithiri kwa migogoro ya ardhi.

**Aidha, aliwaagiza maofisa wa Biashara wa Manispaa ya Shinyanga kuacha tabia ya kufunga biashara za wananchi yakiwamo maduka ambao wamekuwa wakiwadai ko.**

Nipashe
Spotiko



MECHI BORA ZA EPL MAN UTD, LIVERPOOL UK. 12-13



MBAPPE

# WACHEZAJI 10 BORA DUNIANI KWA SASA

**LONDON,** England

HUKU Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wakiwa wameingia kwenye wakati wa mwisho wa maisha yao ya soka, mjadala kuhusu mwanasoka bora wa dunia sasa umekuwa ngumu zaidi.

Kuna nyota wengi duniani kote, huku wachezaji wengi wenye vipaji vingi wakicheza barani Ulaya, lakini linapokuja suala la kulinganisha wale bora, uwanja wa kucheza ni wa kiwango zaidi.

Hapa 90min inawaangalia wachezaji 10 bora duniani kwa sasa - na orodha hii ni sahihi kabisa, kwa hiyo usijisumbue kulalamika...

### #10. Lautaro Martinez

Huku Inter Milan ikielekea kutwaa taji lingine la Ligi Kuu Italia, Serie A, Martinez anatazamiwa kumaliza msimu huu akiwa mfungaji bora wa ligi hiyo.

Fowadi huyo wa Argentina huwa na tabia ya kuwa moto na baridi wakati fulani, lakini amekuwa mtu asiyechoka kabisa katika jezi ya rangi nyeusi na buluu ya Inter kwa muda mwingi wa msimu huu.

### #9. Virgil van Dijk

Beki bora zaidi wa soka duniani kwa sasa, Van Dijk amerejea katika kiwango bora kabisa akiwa na Liverpool mwaka huu huku 'Wekundu' hao wakiwania ubingwa wa Ligi Kuu England.

Mholanzi huyo, ambaye sasa ni nahodha wa 'Wekundu' hao, alifunga bao la ushindi kwenye fainali ya Kombe la Carabao mapema msimu huu na amekuwa nguzo ya kikosi cha Jurgen Klopp msimu wote.

### #8. Vinicius Junior

Vinicius Junior ana ubora wa kucheza pamoja na baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani kote, lakini Mbrazil huyo ni muhimu kwa Real Madrid mabingwa mara 14 wa Ulaya.

Kasi na ujanja wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, humfanya beki wa pembeni kuwa ndoto mbaya na amethibitisha kuwa anaweza kucheza kama sehemu ya wachezaji wawili wa mbele chini ya Kocha Carlo Ancelotti msimu huu.

### #7. Rodri

Man City inapopoteza - ambapo ni nadra kutokea - ni kawaida kwa sababu Rodri hahusiki. Mhispania huyo ni mharibifu katika safu ya kiungo ya ulinzi, lakini pia ana uwezo wa kuchagua safu ya ulinzi na kuibua mabao muhimu.

Rodri alifunga bao la ushindi kwa Man City katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, na hivyo kuimarisha nafasi yake katika viunga vya Man City.

### #6. Harry Kane

Kane hakuchukua muda kuzoea maisha ya Bavaria, haraka akapata mguso wake wa mabao baada ya kuhamia Bayern kutoka Tottenham Hotspur msimu wa majira ya joto.

Nahodha huyo wa England bado anaweza kuvunja rekodi ya Lewandowski ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja wa Bundesliga na amejipendekeza kwa haraka kwa mashabiki wa Allianz Arena - hata kama laana yake ya kutotwaa taji inaonekana itaendelea.

### #5. Mohamed Salah

Salah anaihakikishia Liverpool mabao na hata amekuwa mtoa huduma muhimu kwa wachezaji wenzake kadri anavyozeeka. Licha ya kuwa sasa amefikisha mabao 31, Mmisri huyo anaendelea kutawala orodha ya wafungaji wa 'Wekundu' hao.

Huku wachezaji wenzake wa zamani, Sadio Mane na Roberto Firmino wakiwa wameondoka Anfield, Salah sasa anaweza kufurahia mashabiki wa Liverpool.

### #4. Erling Haaland

Haaland alivunja rekodi ya mabao kwa msimu mmoja wa Ligi Kuu England wakati wa msimu wake wa kwanza Man City, akifunga mara 36 katika mechi 35 kwa mabingwa hao msimu uliopita.

Raia huyo wa Norway anaweza asiwe mwanasoka mwenye kipaji kikubwa cha ufundi zaidi kuwahi kutokea duniani, lakini ukatili wake mbele ya lango unamfanya kuwa miongoni mwa nyota wakatili zaidi duniani.

### #3. Kevin De Bruyne

Jeraha kubwa mwanzoni mwa kampeni ya sasa lilimweka nje De Bruyne kwa miezi kadhaa, lakini alipata miguu yake haraka baada ya kukaa nje kwa muda mrefu na sasa amerejea kwenye ubora wake wa umeme katika kikosi cha Guardiola.

Mbelgiji huyo anaweza kufanya mambo na soka ambalo hakuna mchezaji mwingine anayeweza, kwa pasi yake isiyo na kifani katika soka la dunia.

### #2. Jude Bellingham

Kulikuwa na alama za kuuliza juu ya jinsi Bellingham angeweza kutulia haraka Real Madrid baada ya mabadiliko yake ya msimu wa majira ya joto, lakini aliwanyamazisha wenye shaka wowote ndani ya mechi zake chache za kwanza pale Bernabeu.

Muingereza huyo amefunga mabao mengi muhimu kwa vinara hao wa LaLiga msimu huu na tayari ni mmoja wa viungo bora zaidi duniani akiwa na miaka 20 pekee.


### #1. Kylian Mbappe

Mbappe anakaribia kuungana na Bellingham katika mji mkuu wa Hispania msimu ujao, huku Mfaransa huyo akiwa katika kiwango cha hali ya juu kabla ya kuhamia Real.

Mshambuliaji huyo amekuwa na wastani wa takriban bao moja kwa kila mechi katika kampeni hii hadi sasa na Paris Saint-Germain mara nyingi imekuwa ikisumbuka bila yeye kwenye timu. Atakuwa hasara kubwa kwao muhula ujao, lakini hasara yao itakuwa faida kubwa kwa Real Madrid.

## ISIKUPITE

USHINDI wa mabao 3-0 Arsenal iliyoupata dhidi ya Brighton juzi, unaifanya sasa kushinda mechi 10 kati ya 11 zilizopita za Ligi Kuu England ikizoa pointi 31 kati ya 33 zinazowezekana mwaka 2024, na kufunga jumla ya mabao 38 huku ikiruhusu manne tu katika mechi hizo.






Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah na kiungo wa Machester United, Bruno Fernandes, timu hizo zilipokutana kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita. **PICHA: MTANDAO**

# MECHI BORA ZA EPL MAN UTD, LIVERPOOL

**LONDON,** England

MABUSU ya kamera, mateke ya juu, wachezaji wa akiba waliotolewa nje na mechi za kwanza za kukumbukwa - mechi kati ya Manchester United na Liverpool imekuwa na kila kitu.

**Wakiwa wametoka kwenye mchezo wa kusisimua wa Kombe la FA, wawili hao jana Jumapili walikutana tena kwenye Ligi Kuu England.**

Huku mchezo wa jana ukiwa na mchango mkubwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu kwa Liverpool na nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwa Man United, hapa tunakuletea baadhi za mechi za kusisimua za Ligi Kuu kati ya timu hizo mbili, twende sasa...

### Liverpool 3-3 Manchester United - Januari 1994

Tutaanza katika msimu wa pili baada ya maboresho ya Ligi na kuitwa Ligi Kuu England, wakati mabingwa watetezi Manchester United walipoongoza kwa mabao 3-0 ndani ya dakika 25 wafungaji wakiwa Steve Bruce, Ryan Giggs na Denis Irwin.

Man United walionekana kumweka roho juu Kocha wa Liverpool, Graeme Souness, lakini timu yake ilijizatiti na kurudi kwenye mchezo baada ya Nigel Clough kufunga mabao mawili.

Katika kipindi cha pili Liverpool walikamilisha mchezo ambao haukutarajiwa kwa sare baada ya bao la kichwa la Neil Ruddock dakika 11 kabla ya mchezo kumalizika.

Hata hivyo, Man United walikuwa na kicheko cha mwisho kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 32 zaidi ya Liverpool - ambao walimaliza katika nafasi ya nane.

Kuhusu Souness, kichapo cha Kombe la FA kutoka kwa Bristol City kilimfanya ajiuzulu wiki chache baada ya mchezo huo pale Anfield.

### Manchester United 1-4 Liverpool - Machi 2009

Kulikuwa na mechi nyingi za kuvutia kati ya wawili hao, lakini mambo hayakuwa motomoto kwenye ligi hadi mwaka 2009.

United walionekana kuwa tayari kwenda kwa pointi 10 mbele ya Liverpool waliokuwa nafasi ya pili wakati Cristiano Ronaldo alipowapatia uongozi wa mapema kwa mkwaju wa penalti kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Lakini wageni walibadilisha mambo kupitia Fernando Torres na mbusu kamera, Steven Gerrard.

Torres alimtawala Nemanja Vidic wa United katika mchezo wote, huku beki huyo akitolewa nje kwa kadi nyekundu na Fabio Aurelio akafunga kwa mkwaju wa faulo, kabla ya Andrea Dossena kufunga bao la nne baadaye.

United iliaibishwa Old Trafford lakini mwisho wa msimu waliifikia rekodi ya Liverpool ya mataji 18 ya Ligi Kuu, wakimaliza kwa pointi nne mbele ya Wekundu wa Anfield hao.

### Manchester United 3-2 Liverpool - Septemba 2010

Mwaka mmoja baadaye Manchester United ililipiza kisasi zaidi kutokana na uchezaji mzuri wa namba tisa wao, Dimitar Berbatov.

Mshambuliaji huyo raia wa Bulgaria alifunga kila kipindi.

Hata hivyo, Liverpool walionekana kuwa imara kwa mabao mawili ya Gerrard, ambaye alifunga mara mbili ndani ya dakika sita, kabla ya Berbatov kukamilisha hat-trick yake kwa kufunga kwa kichwa dakika ya 84.

United walishinda ligi msimu huo, lakini wakashindwa katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Barcelona.

Liverpool iliyokuwa chini ya kocha, Roy Hodgson ilimaliza katika nafasi ya sita, pointi 22 nyuma ya wapinzani wao.

### Liverpool 1-2 Manchester United - Machi 2015

Liverpool walifunga mabao mawili dhidi ya Manchester United ya David Moyes msimu wa 2013-14, lakini wakachapwa katika msimu uliofuata.

Nahodha Steven Gerrard alitolewa nje kwa kadi nyekundu sekunde 38 baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba katika kipindi cha pili, katika mechi iliyojumuisha mkwaju mzuri wa Juan Mata.

Gerrard aliingia kuchukua nafasi ya Adam Lallana mwanzoni mwa kipindi cha pili, huku United ikiongoza kupitia bao la mapema la Mata. Lakini alitolewa nje kwa kadi nyekundu haraka baada ya kumkanyaga Ander Herrera wa United.

Katika kipindi cha pili chenye machafuko, Mata aliiongezea United bao la pili kwa shuti kali, na Daniel Sturridge akafunga bao la kufutia machozi, na Wayne Rooney wa United kisha akakosa penalti ya dakika za lala salama iliyookolewa na Simon Mignolet.

'Mashetani Wekundu' hao walimaliza msimu wa kwanza wa Louis van Gaal katika nafasi ya nne, pointi nane zaidi ya Liverpool iliyoshika nafasi ya sita ikiongozwa na kocha Brendan Rodgers.

### Liverpool 7-0 Manchester United - Machi 2023

Ushindi wa mabao 7-0 wa Liverpool ulikuwa mkubwa zaidi katika historia ya mchezo huo, na kupita ushindi wa 7-1 wa Wekundu hao katika mchezo wa Ligi Daraja la pili msimu wa 1895-96.

Liverpool wakiwa na mchezo mzuri - ambao ulimjumuisha Mohamed Salah na kumfanya kuwa mfungaji bora wa Klabu kwenye Ligi Kuu.

Cody Gakpo aliwaweka wenyeji mbele kwa bao 1-0, huku Darwin Nunez akifunga dakika mbili baada ya kipindi cha pili na kufungua milango ya mafuriko ya mabao.

Hatimaye Gakpo, Nunez na Salah wote walifunga mawili, huku Roberto Firmino akikamilisha bao la saba dakika ya 88 na kupata ushindi mkubwa zaidi katika historia ya mchezo huo.

Hiyo ilikuwa ni saba baada ya Man United ya Erik ten Hag kushinda Kombe la Carabao.

Walimaliza msimu wa wakiwa nafasi ya tatu, huku Liverpool wakiwa wa tano.

### Baadhi ya mechi nyingine za kuvutia kwa timu hizo

Manchester United 2-2 Liverpool - Oktoba 1995 - Eric Cantona alicheza mchezo wake wa kwanza baada ya kufungiwa kwa miezi nane, akifunga bao la kusawazisha dakika za mwisho kwa United.

### Liverpool 2-3 Manchester United - Septemba 1999

Jamie Carragher alifunga mabao mawili ya kujifunga wakati United ikishinda pale Anfield.

### Manchester United 3-1 Liverpool - Septemba 2015

Anthony Martial alifunga bao lake la kwanza katika mechi ya mwisho ya Rodgers dhidi ya United kama kocha wa Liverpool.

### Manchester United 0-5 Liverpool Oktoba 2021

Mechi ya kiwango ilioneshwa kikamilifu, huku Mohamed Salah akipiga hat-trick na kuongeza shinikizo zaidi kwa kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer.

### Liverpool 4-0 Manchester United - Aprili 2022

Na katika msimu huo huo Liverpool walifunga mabao mengine manne bila majibu pale Anfield, dhidi ya timu ya United iliyokuwa inaongozwa na kocha wa Ralf Rangnick.

## Nukuu



"Kupigania taji moja ambalo haujashinda kwa miaka mingi ni 'wow, ni rahisi'. Lakini sasa kwa miaka mingi, bado kuna [kushindana] ni 'wow'. Kigezo cha vizazi vipya kwa klabu hii, kwa kile tulichofanya ni kizuri sana," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akiamini kuwa Arsenal kupigania ubingwa wa Ligi Kuu England ni rahisi kuliko klabu yake kuutwaa kwa mara ya nne.**




"Nadhani wote wawili ni wa kushangaza. Tunazungumza juu ya wachezaji wawili bora, si tu ulimwenguni, lakini historia ya mchezo huu. Siku zote nilisema Messi ana kipaji ambacho hakuna mtu anacho. Cristiano Ronaldo ni mchezaji tofauti sana, wanatofautiana sana [na Lionel Messi], ni mrefu, ana nguvu, amekamilika kweli kweli. Anaweza kufanya lolote. Anaweza kufunga magoli kwa kichwa, free-kick, penalti, moja kwa moja. Kwangu mimi, ni kama Messi si binadamu, lakini Cristiano ni binadamu bora zaidi," **Beki wa zamani wa Barcelona, Gerard Pique, kuhusu mjadala wa nani bora kati Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.**



"Alikuwa na kila kitu, aliweza kupiga chenga, alikimbia nyuma, aliweza kuruka na kupiga mpira kichwa, aliweza kuingia ndani, akatoka nje. Kwa hiyo nasema siku zote alikuwa akinipa wakati mgumju, lakini unajaribu kufanya kazi kila mmoja nje na tulipata kilicho bora zaidi wakati mwingine," **Beki wa zamani wa Chelsea, Ashley Cole, akielezea kuwa Cristiano Ronaldo, ndiye mshambuliaji aliyempa wakati mgumu zaidi kumkaba katika historia yake kisoka.**

# USIYOYAJUA SIMBA, YANGA MECHI ROBO FAINALI CAF



Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akipambana kumdhibiti winga wa kushoto wa Al Ahly ya Misri, Hussein E Shahat, katika mechi ya robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyochezwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, nchini Misri, Wekundu wa Msimbazi wakipoteza kwa mabao 2-0, na kuondolewa kwa jumla ya mabao 3-0, baada ya kufunga bao 1-0 nyumbani.

**Na Adam Fungamwango**

IJUMAA iliyopita haikuwa siku nzuri kwa Watanzania, baada ya kuzishuhudia timu zao, Simba na Yanga zikisukumizwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, hatua ya robo fainali.

**Saa 3:00 usiku, Yanga ikiwa Bondeni, Afrika Kusini, Uwanja wa Loftus Versfeld jijini Pretoria, ilicheza mechi yake dhidi ya wenyeji wao, Mamelodi Sundowns, na iliisha kwa miamba hiyo ya Tanzania kufungwa kwa penalti 3-2.**

Timu hizo zililazimika kwenda kwenye hatua hiyo baada ya kutoka suluhu katika mechi hiyo, lakini pia hata Machi 30, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hazikufungana.

Wakati Watanzania wakiwa na majonzi, saa 5:00 usiku ilichezwa mechi nyingine ya robo fainali ya michuano hiyo, Simba ikiwa ugenini pia dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri, mechi ikipigwa Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, Misri.

Wawakilishi hao wa Tanzania nao waliondolewa kwa kufungwa mabao 2-0 katika mechi hiyo, ambapo Machi 29, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, walifungwa bao 1-0, hivyo kutupwa nje kwa jumla ya mabao 3-0.

Katika makala haya tumekukusanyia matukio yote ya mechi zote mbili, rekodi na takwimu, tukiziweka katika mtindo wa namba.

**#521.** Hii ni idadi ya pasi zilizopigwa na Simba katika mechi yao ya Ijumaa iliyopita dhidi ya Al Ahly, ikiwa ni idadi ya juu zaidi ya zote zilizopigwa katika mechi zote mbili zilizozihusu timu za Tanzania na wapinzani wao.

**517#.** Ni idadi ya pasi zilizopigwa na Mamelodi Sundowns katika mechi ya Ijumaa ilipocheza dhidi ya Yanga, ikiwa ni pungufu ya pasi nne tu ya zile zilizopigwa na Simba katika mechi yao dhidi ya Al Ahly.

**#414.** Al Ahly ilipiga idadi hii ya pasi katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Simba.

**#182.** Idadi hii ya pasi zilizopigwa na Yanga katika mechi dhidi ya Mamelodi Sundowns, ikiwa ni za chini zaidi ukijumlisha timu zote nne za wawakilishi wa Tanzania na wapinzani wao.

**#90.** Simba ilifungwa bao la pili dakika hii ya mchezo kwa mkwaju wa penalti iliyowekwa wavuni na Mahmoud Karhaba, baada ya mchezaji mmoja wa timu hiyo kufanyiwa madhambi na Fondoh Che Malone ndani ya eneo la hatari.

**#74.** Ni asilimia za umiliki wa mpira kwa timu ya Mamelodi Sundowns ilipocheza dhidi ya Yanga, Ijumaa nchini Sauzi.

**#56.** Simba ilimiliki mpira kwa asilimia hizi katika mechi yao iliyocheza Cairo na kuwazidi wapinzani wao waliokuwa nyumbani.

**#47.** Ni dakika ambayo Simba iliruhusu bao la kwanza lililowekwa wavuni na Amr El Solia kutokana na uzembe mkubwa wa mabeki wa Simba ulioanzia kwa Shomari Kapombe, huku viungo wakabaji nao wakichelewa kuja kuwasaidia mabeki wa kati kukaba wapinzani waliokuwa huru, baada ya kipa Ayoub Lakred kuuokoa mpira, na kumkuta mfungaji aliyekuwa hajakabwa kabisa.

**#44.** Ni asilimia za umiliki wa mpira kwa Al Ahly dhidi ya Simba katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa iliyochezwa Ijumaa iliyopita jijini Cairo.

**#26.** Yanga ilimiliki mpira kwa asilimia hizi katika mechi ya robo fainali Ijumaa iliyopita dhidi ya Mamelodi Sundowns.

**#19.** Idadi ya faulo zilizochezwa na Yanga katika mechi hiyo iliyoisha kwa wenyeji kusonga mbele kwa mikwaju ya penalti.

**#17.** Simba ilicheza idadi hii ya faulo katika mechi yao dhidi ya Al Ahly, ikiwa ni pungufu ya mbili tu dhidi ya Yanga iliyocheza na Mamelodi Sundowns.

**12#.** Hizi ni idadi ya faulo zilizochezwa na wachezaji wa Al Ahly dhidi ya Simba katika mechi hiyo.

**#10.** Jumla ya mashuti yaliyopigwa na Simba katika mechi yao dhidi ya Al Ahly, ambapo kati ya hayo ni mawili tu yaliyolenga lango.

**#9.** Mamelodi Sundowns ilicheza faulo mara idadi hii, ikiwa ndiyo timu iliyocheza madhambi mara chache zaidi katika mechi hizi mbili zilizokuwa zikitazamwa sana na Watanzania.

**#8.** Idadi ya wachezaji wa kigeni wa Simba walioanza kwenye mechi ya Ijumaa iliyopita dhidi ya Al Ahly ikipoteza kwa mabao 2-0.

Mapro hao ni Mmorocco Ayub Lakred, Mzambia Clatous Chama, Mrundi Saido Ntibazonkiza, Fabrice Ngoma na Inock Inonga raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Sadio Kanoute kutoka Mali, Babakar Sarr wa Senegal, na Che Malone, raia wa Cameroon.

**#7.** Namba hii ni jumla ya mashuti yaliyopigwa na wachezaji wa Al Ahly kuelekea kwenye lango la Simba, huku manne yakilenga lango.

**#6.** Yanga ilianza na idadi hii ya wachezaji wa kigeni kwenye mechi yake ya Ijumaa dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Wachezaji hao ni Stephane Aziz Ki raia wa Burkina Faso, Djigui Diarra (Mali), Joyce Lomalisa na Maxi Nzengeli kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Kennedy Musonda (Zambia) na Joseph Guede rai wa Ivory Coast.

**#5.** Idadi ya wachezaji wa Kitanzania wa Yanga walioanza katika mechi dhidi ya Mamelodi Sundowns, ambao watatu wakiwa mabeki wa wawili ni viungo wakabaji. Wachezaji hao ni Job, Bakari Mwamnyeto, 'Bacca', Mudathir Yahaya na Jonas Mkude.

Pia, namba hii inasimama kuwa ni idadi ya wachezaji wa Yanga walioonyeshwa kadi za njano katika mechi hiyo, ambao ni Lomalisa, Job, Bacca, Nzengeli na Mudathir.

**#3.** Idadi ya wachezaji wa Kitanzania walioanza kwenye mechi kati ya Simba dhidi ya Al Ahly, ambao ni Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Kibu Denis.

Namba pia inasimama kwa jumla ya penalti zilizofungwa na kuiondoa Yanga kwenye michuano hiyo, zikiwekwa wavuni na Marcelo Allende, Lucas Ribeiro na Neo Maema.

**#2.** Namba hii inasimama kwa timu zote Simba na Yanga kuwa na wachezaji wawili wawili kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambao wote walianza.

Wakati Yanga ikiwa na Lomalisa na mwenzake Nzengeli, Simba ilikuwa na Inonga na Ngoma.

Namba hii pia inasimama kwa mabao ya penalti ambayo Yanga ilitumbukiza wavuni ingawa hayakutosha kuwavusha, yakifungwa na wachezaji wote kutoka Afrika Magharibi, Guede wa Ivory Coast na Augustine Okra raia wa Ghana.

**#1.** Simba na Yanga zilikuwa na wachezaji mmoja mmoja wanaotoka kwenye taifa moja. Wakati Simba ikiwa na Chama kutoka Zambia, Yanga ilikuwa na Musonda wa nchini humo, huku Wanajangwani hao wakiwa na Diarra kutoka Mali, Simba ilikuwa na Kanoute wa nchi hiyo.

Namba hii inasimama kama idadi ya kuotea kwa timu zote mbili za Mamelodi Sundowns na Yanga.

**0#.** Namba hii inasimama kwa Yanga na Mamelodi kutopata bao ndani ya dakika 90 katika mechi zote mbili.

## JE, WAJUA?



USHINDI wa mabao 7-0 Liverpool ilioupata dhidi ya Manchester United Machi 2023 kwenye Ligi Kuu, ndio mkubwa zaidi katika historia ya mchezo huo dhidi ya timu hizo, huku ukipita ule wa United ilipowachapa 'Majogo wa Anfield' 7-1 kwenye Ligi Daraja la Pili msimu wa 1895-96. Mabao ya Liverpool siku hiyo yalifungwa na Cody Gakpo (43' na 50'), Darwin Nunez (47' na 75'), Mohamed Salah (66' na 83'), Robert Firmino (dk. 88)



# Miradi ya bilioni 141/- yawekezwa Chamwino, miaka 3 ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

KATIKA kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, serikali imewekeza miradi mbalimbali wilayani Chamwino mkoani Dodoma yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 141.

Mkuu wa wilaya ya Chamwino, Janeth Mayanja, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa wilaya hiyo kwenye mkutano wa kumpongeza Rais Samia kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake.

Mayanja aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuitunza, kuilinda miradi mbalimbali iliyowekezwa kwa kiasi hicho cha fedha ili iwe na tija kwa taifa.

Alisema, serikali imewekeza mabilioni hayo ya fedha kwa ajili ya sekta mbalimbali, hivyo wananchi wanatakiwa kuitunza, kuilinda kwa gharama yoyote na kwa kufanya hivyo watakuwa wamemuunga mkono Rais katika jitihada za kuleta maendeleo nchini.

"Nitoe rai kwa wananchi wa Wilaya ya Chamwino msimwangushe Rais Samia kutokana na uwekezaji huo mkubwa wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekelezwa kwenye meneo yenu kuanzia kwenye kata, vijiji hadi kwenye vitongojini huko.

Aliwataka wataalam na watendaji kuhakikisha wanatembelea miradi hiyo kwenye maeneo ambayo imewekezwa badala ya kukaa ofisini na kusubiri kuletewa taarifa, hali ambayo inaweza kusababisha kutokukamilisha kwa wakati na wananchi watakosa imani juu ya uwekezaji huo.

Hivyo, aliwataka kuweka wazi thamani ya miradi inayotekelezwa kwa wananchi na kipindi walichokiweka hadi kukamilika kwake ili wananchi waweze kutambua badala ya kuiendesha kwa uficho.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Tito Mganwa, alisema fedha walizozipata zitahakikisha zinakamilisha miradi yote.

Mganwa alisema kuna miradi mingi ambayo inatekelezwa hivi sasa ikiwemo ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, shule za msingi na sekondari, umeme, maji kilimo, ufugaji na maji.



# Serikali yatoa maagizo manne uhamasishaji Dira ya Maendeleo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa maagizo manne kwa makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa ya kuhamasisha utoaji maoni ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, ambapo kaya 7,800 zinatarajiwa kuhojiwa.

Aidha, shughuli za ukusanyaji maoni zitahitimishwa Novemba 30, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kufanyika mikutano kadhaa ya viongozi.

Akizungumza jana kwenye kikao cha viongozi hao kuhusu ukusanyaji maoni hayo kilichoratibiwa na Tume ya Mipango, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof.Kitila Mkumbo, alisema katika maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa sekretarieti za mikoa ni kuhakikisha zinatoa ushirikiano na zisaidie tume hiyo kuwafikia wananchi wengi katika ukusanyaji maoni.

Aliagiza tume kutoa ratiba kwenye mikoa ili kujiandaa itakapofikiwa na timu ya wataaalamu wa kukusanya maoni hayo.

"Tupo katika mchakato mkubwa wa nchi yetu wa pili wa kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo tunatarajia itupeleke miaka mingine 25 au zaidi, Dira ya miaka 25 ni kidogo nchi nyingi zinazungumzia hadi miaka 100, pengine inawezekana kuongeza muda na Rais alishatoa kibali," alisema.

Alisema wanapokusanya maoni yatalenga zaidi ya miaka 25 na kusisitiza viongozi hao watano kuzingatia misingi mitano iliyotajwa na Rais Samia ikiwamo ushirikishwaji wa wadau wote muhimu.

"Kuna kushirikisha wananchi wote na wadau wote muhimu, kwa hiyo kwenye mikoa yenu mtusaidie kutambua makundi yote muhimu ambayo wataalamu wetu wakija watakutana nayo na kufanya mahojiano ili kupata maoni yao," alisema.

Alisema Rais Samia amesisitiza kila mwananchi hapa nchini na wale waliopo ughaibuni washiriki kikamilifu katika uandishi wa dira hiyo mpya.

Hata hivyo, alisema yataandaliwa makongamano kwenye mikoa mbalimbali ili wadau na wananchi watoe maoni yao na tukio la mwisho la kuhitimisha mchakato huo lifanywa Novemba 30, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Dk.Tausi Kida alisema viongozi hao ni wadau muhimu katika kufanikisha ukusanyaji wa maoni ya dira hiyo itakayoendeleza hatua za maendeleo zilizotokana na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025.

Naye, Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Lawrance Mafuru alisema baada ya ukusanyaji wa maoni watarudi tena kwa wananchi kuwaonyesha kabla ya kuchapisha ili waseme sawa au kama kuna kilichoachwa.

Alisema mbinu zitakazotumika kuwafikia watu wengi ni mahojiano ya ana kwa ana, ujazaji wa dodoso kupitia simu za mkononi, mikutano kama vile malumbano ya hoja, makongamano na mitandao ya kijamii.

Alifafanua orodha ya kaya itachukuliwa kwenye kanzi data ya Sensa ya Watu na Makazi na halmashauri mbili zimechaguliwa kwa kila mkoa, kata mbili kwa kila halmashauri, kaya 60 zitahojiwa kwa kata.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akiwa na watoto yatima wa kituo cha Zamzam cha Miyuji, baada ya kuwakabidhi msaada wa chakula uliotolewa na Benki ya NMB, katika hafla ya futari iliyofanyika Bungeni, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede (kulia) na (kushoto) ni Ofisa Mkuu wa fedha wa benki hiyo, Juma Kimori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukosefu elimu ya bima bado tatizo kwa Watanzania

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKOSEFU wa elimu ya bima ya mali na vyombo mbalimbali kwa Watanzania, kumetajwa kuwa moja ya sababu ya watu wengi kushindwa kutambua umuhimu wake hali iyochangia kwa kiasi kikubwa kupata hasara pindi wanapopatwa na majanga mbalimbali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya wkala wa bima zinazozingatia sheria za dini ya kiislam ya Wema Takaful, Ally Ally alibainisha hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akizungumzana na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa bima ya mali.

Alisema moja ya shida iliyopo nchini ni elimu ya masuala ya bima ya mali mbalimbali kwa wananchi hali ambayo inasababisha watu wengi kushindwa kutambua umuhimu wake.

"Kukosekana kwa elimu ya bima za mali kwa watu wengi ndiko kumekuwa chanzo cha watu kushindwa kuwa na bima kutokana na kutotambua umuhimu wake, hivyo unakuta watu wanamiliki nyumba, magari lakini hawana bima ya majanga.

Alisema, kutokana na hali hiyo anaishauri serikali kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya masuala ya bima za mali ili kusaidia wananchi wengi ambao wamekuwa wakipata hasara ya mali zao kila yanapotokea majanga.

"Katika mataifa mengine bima ni jambo la lazima lakini leo hii hapa kwetu kutokana na watu kukosa elimu unakuta mtu anaweza kuingiza hata gari lake barabarani bila kuwa na bima na linapopata shida kama vile kupata ajali hakuna ambachopata zaidi ya hasara ya mali yake" alisema

Aidha, alisema ipo haja kwa serikali kuona umuhimu wa somo la bima kuanzia ngazi ya shule za msingi ili kuwajengea Watanzania uelewa wa umuhimu wa kuwa na bima za mali na vyombo mbalimbali.

Akizungumzia kuhusu huduma za bima zinazofuta sheria za kiislam alisema ni msaada kwa waamini wa imani hiyo ambao wamekuwa wakishindwa kukata zile za kawaida kwa kuhofia mambo mbalimbali ikiwemo riba ambayo ni kinyume na imani zao.

"Bima hii inayofuata sheria za dini ya kiislamu inasaidia watu wenye imani hii kuwa na bima bila kuhofia kuharibu imani zao kutokana na zile zingine ambazo labda zimekuwa na masuala ya riba ndani yake au fedha zile kutumika katika mambo mengine ambayo ni kinyume na imani ya kiislam" alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Shekhe Ahmed Saidi, alisema kwa mujibu wa dini ya kiislam suala la riba ni haramu, hivyo uwepo wa bima hiyo inayozingatia sheria ya dini za kiislamu kutasaidia waumini wengi kukatia mali zao bima ili kujiepusha na hasara zitokanazo na majanga mbalimbali.





# Mbaroni tuhuma za kubaka mwanafunzi shule ya msingi

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Edger Mkane (23) mkazi wa Mtaa wa Kisiwani Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa darasa la saba (11) kwa kuahidi kumpa shilingi 1,500.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga aliliambia Nipashe kwa njia ya simu kwamba tukio hilo limetokea Aprili, 04 mwaka huu majira ya saa nane mchana.

Alisema mtuhumiwa na mwanafunzi anayedaiwa kubakwa ni mtu na binamu yake, hivyo mwanafunzi huyo alikwenda kuangalia televisheni nyumbani kwao na mtuhumiwa ndipo tukio hilo likatendeka.

Alisema tukio hilo kidaktari halijathibitika, hivyo kuleta ukinzani kati ya taarifa inayotolewa na daktari na ile inayotolewa na wahusika.

Alisema daktari alieleza kuwa vipimo havionyeshi kuwa mwanafunzi huyo ameingiliwa, lakini mwathirika na mtuhumiwa wanakubali kufanyika kwa tukio hilo.

"Haya sisi tunaita mashambulio ya aibu kwamba mtu anamshika mwanamke au kushika uume wake kugusisha pale lakini tukio la ubakaji linakuwa halijakamilika," alisema Banga.

Banga alisema jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi juu ya tukio hilo na kuahidi kufikia sehemu nzuri na ikithibitika sheria itafuata mkondo wake.

Awali, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kisiwani, Rajabu Shayo alisema jamii inatakiwa kuacha tabia ya kumaliza matatizo ya aina hiyo kifamilia kwani imekuwa ikichangia kuendelea kwa matukio hayo ya kikatili kwa watoto.

"Hili tukio nimelipokea kwa masikitiko sana kinachonisikitisha zaidi huyu mtu siyo mara yake ya kwanza mimi nimeshuhudia mara mbili na aliwahi kupelekwa polisi, mama yake alinifuata na kulalamika mtoto wangu anaonewa," alisema Shayo.

Mtuhumiwa wa tukio hilo, Edger Mkane alisema sababu ya kumbaka mtoto huyo ambaye ni binamu yake ni tamaa na kueleza kuwa mtoto huyo aliendа nyumbani kwao ili kuangalia televisheni na kumuahidi kuwa atampa Sh. 1,500 endapo takubali kufanya naye tendo hilo.

Naye mwanafunzi huyo amekiri kufanyiwa kitendo hicho na kueleza kuwa aliendа nyumbani kwa shanganzi yake kuangalia televisheni ndipo mtuhumiwa akajaribu kumshawishi licha kuwa alikataa.

Mzazi wa mtoto huyo aliiomba serikali kumchukulia hatua za kisheria mtuhumiwa huyo ili iwe fundisho kwa watu wengine ambao wanajihusisha na vitendo vya ubakaji.



Mratibu wa mafunzo wa Barrick Tanzania, Elly Shimbi, akizungumza na wanafunzi wa vyuo vikuu, wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo wa kuhimili ushindani wa ajira na kujiajiri lililoandaliwa na taasisi ya kuchipua na kuendeleza vipaji vya uongozi kwa vijana (AIESEC), kwa udhamini wa Barrick katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima watakiwa kuacha kulalamika kuhusu bei ya mazao

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WAKULIMA katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe wametakiwa kuachana na malalamiko kuhusu bei ya mazao na badala yake wazingatie maelekezo ya wataalamu, ili kupata tija katika kilimo chao.

Kauli hiyo imekuja baada ya wakulima walio wengi kuendelea kulalamikia kuhusu bei ndogo ya mazao wakati wanachozalisha hakina tija kutokana na kutumia eneo kubwa la shamba kuzalisha kiasi kidogo cha mazao, hivyo kushindwa kumudu gharama za uendeshaji

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Beatrice Tarimo wakati wa uzinduzi wa duka la pembejeo za kilimo One Acre Fund uliofanyika katika halmashauri hiyo wilayani Njombe.

Alisema wakulima walio wengi wamekuwa wakilalamikia bei ya mazao lakini changamoto kubwa iliyopo kwa Watanzania katika kilimo siyo bei bali ni tija katika kile kinachozalishwa.

"Uzalishaji kwa eneo mkulima anasema bei ya mazao ni ndogo kwa sababu kama kwenye ekari moja amevuna gunia nne akaenda kuziuza Sh. 30,000 maana yake atapata sh. 120,000 ukilinganisha gharama za uzalishaji na alichokipata hakiendani kwahiyo kwa haraka haraka mkulima atakwambia shida yetu kubwa ni bei ya mazao," alisema Tarimo.

Tarimo alisema wakulima wanatakiwa kuondokana na tatizo la bei kwa kuanza kupambana na tatizo la tija katika kile ambacho kinazalishwa na wakulima.

Alisema katika kupambana na tatizo la tija wakulima wanatakiwa kupata pembejeo kwa wakati ikiwemo mbolea, mbegu pamoja na viwatilifu.

Hata hivyo Tarimo alisema ili kilimo kiwe endelevu wakulima wanatakiwa kuchukua hatua kwa kulima kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Ofisa Kilimo kutoka kitengo cha pembejeo katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Peter Emmanuel alisema ili wakulima wapate tija ya kile wanachozalisha wanatakiwa kufuata kanuni za kilimo ikiwemo kuundaa shamba mapema kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Ofisa Uhusiano kutoka One Acre Limited Tanzania, Enhart Israel alisema uzinduzi wa duka hilo la pembejeo za kilimo utaleta chachu na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa urahisi.

Diwani wa Kata ya Kitisi, Halmashauri ya Mji Makambako, Navy Sanga alisema uzinduzi wa duka hilo la pembejeo limewasaidia wananchi wa kata hiyo ambao awali walilazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo hadi Njombe Mjini.

## Wafanyabiashara wapewa mbinu utatuzi changamoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIBU Tawala Msaidizi wa Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mkoa wa Mbeya, Anna Mwambene amewaasa wafanyabiashara kulitumia Baraza la Ushindani (FCT) katika kutatua changamoto za kibiashara zilizotolewa maamuzi na mamlaka za udhibiti au tume ya ushindani.

Alitoa ushauri huo juzi alipokuwa akifungua semina ya elimu kwa wadau wa FCT iliyofanyika jijini Mbeya.

Akiwa anatoa mafunzo hayo Mkuu wa Idara ya Uchumi katika baraza hilo, Kulwa Msogoti alisema kuwa baraza hilo lilianzishwa chini ya Kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Aidha, Msogoti alieleza kuwa baraza hilo lilianzishwa kwa dhumuni la kukuza na kulinda ushindani wenye tija katika soko na kuzuia mwenendo na tabia potofu katika soko la Tanzania, ili kuongeza ufanisi na uzalishaji, usambazaji wa huduma na bidhaa, kukuza ubunifu, kuwezesha matumizi ya rasilimali yenye ufanisi na kumlinda mlaji.

Msogoti alisema dhumuni hilo linatekelezwa kwa kushughulikia migogoro ya wafanyabiashara, wawekezaji, watoa huduma na walaji ikiwemo jamii inayohusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko kwa njia ya kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za rufaa.

Msogoti alisema baraza hilo hupokea, kusikiliza na kuamua kesi za rufaa zinazotokana na maamuzi yaliyotolewa Tume ya Ushindani-FCC, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri na Usalama wa Anga (TCAA).

Zingine ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Mawasiliano na Utangazaji (TCRA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Nishati ya Petroli (PURA).

Aidha, alisema kuwa kuanzia mwaka 2007 hadi machi, 2024 baraza limesajili jumla ya mashauri 442.

"Mashauri 429 sawa na asilimia 97.1 yameshasikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri 13 yaliyobaki yapo kwenye hatua mbalimbali za usikilizwaji," alisema Msogoti.

Msogoti alibainisha kuwa matokeo ya maamuzi ya mashauri hayo yameongeza uwajibikaji kwa wadau wote katika soko na kuchochea kampuni kuongeza umakini katika kufuata sheria za nchi.

Ofisa Sheria Mkuu wa FCT, Hafsa Said alisema kampuni ya biashara au taasisi inaruhusiwa kuwasilisha maombi ya rufaa na lazima ithibitishe kuwa, uamuzi unaoombewa rufaa lazima uwe umefanywa na moja ya mamlaka za udhibiti zilizotajwa hapo awali au Tume ya Ushindani.



# Serikali kuimarisha huduma za uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Shaaban Ali Othman amesema serikali itahakikisha huduma za uvuvi zinaimarika na kuwa bora kama zilivyo huduma nyingine za kijamii.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha makabidhiano ya mtambo wa kuzalisha barafu wenye uwezo wa kuzalisha tani tano kwa siku kwa watumiaji wa Soko la Samaki Malindi.

Waziri Shaaban alisema mtambo huo utawasaidia wavuvi wanaotumia soko hilo kwa kuhifadhia samaki wao na kuondokana na adha ya kutafuta barafu kwa wamiliki wa majokofu binafsi.

Alisema kuwa Serikali ya Zanzibar ikitafuta njia mbadala za kuwasaidia wajasiriamali wakiwemo wavuvi wa samaki kwa kutafuta njia zitakazoondosha changamoto, hivyo kuwepo kwa mtambo huo katika soko hilo kutasaidia wafanyabiashara na wavuvi kuendelea na kazi zao bila kuwa na usumbufu.

Alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuwasaidia wavuvi wadogo kuvua katika kina kirefu cha maji ya bahari kwa kuwapatia mafunzo ya kisasa.

Aidha, aliwataka wavuvi kuutuza mtambo huo ili utumike muda mrefu kwa maslahi yao na taifa.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Dk. Saleh Yahay alisema kampuni ya Albakora inathamini wavuvi wadogo na wa kati na inasaidia shughuli mbalimbali za wavuvi kuondokana na kuvua kwenye maji madogo na kuendeleza uvuvi haramu ambao unaathari kwa nchi.

Alisema mtambo huo unagharimu Sh. milioni 100.3 na utazalisha barafu zaidi ya tani tano za vinoo vya barafu kwa siku.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Zahor Kassim El Gharousy alisema serikali imetoa kipaumbele kwa wavuvi wadogo ili kuimarisha uvuvi wa bahari kuu usipotee.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Albakora kutoka Hispania, Imanol Ioinaz alisema Serikali ya Hispania itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuleta maendeleo ya uvuvi ambapo mashine hiyo itawasaidia wavuvi kuhifadhia samaki waliokuwa bado hawajapelekwa sokoni kwa ajili ya mauzo.

Mwenyekiti wa wauzaji samaki Soko la Malindi, Amour Rashid Amour alisema mtambo huo unawasaidia wavuvi wanaoendesha shughuli zao katika soko hilo kwa ajili ya kuhifadhia samaki na kuondokana na kero za kuharibika kwa mazao ya baharini yanayovuliwa na wavuvi.

# Wawili wafa mtumbwi ukipinduka

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATU wawili wamefariki dunia na wengine watatu kunusurika baada ya mtumbwi waliokuwa wanasafiria katika Mto Kilombero kutoka kambi ya wavuvi ya Iluwa, wilayani Ulanga kuelekea kijiji cha Katindiuka, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro kupinduka na kuzama majini.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara, wilayani Kilombero, Godwin Mukaruka alitoa taarifa hiyo jana baada ya kufika eneo la tukio.

Alisema watu hao walikuwa wanatoka kwenye kambi ya wavuvi jioni ya Aprili 4, mwaka huu.

Alisema kuwa walipoona maji yanazidi kujaa eneo la kambi hiyo, waliamua kuondoka kwa usafiri wa mtumbwi na walipofika katikati ya mto huo, mwendesha mtumbwi alishindwa kuhimili mawimbi ya maji ya mto huo na mtumbwi ukapinduka.

Mukaruka alisema watu wawili ambao ni wanawake walifariki dunia na wengine watatu akiwamo mtoto walifanikiwa kujiokoa.

"Kwa sasa tupo msiba wa watu wawili waliofariki dunia (Aprili 4, 2024) kutokana na maji hayo, walikuwa wanatoka kwenye kambi ya wavuvi, wakirejea nyumbani kwenye maeneo yao," alisema Mukaruka.

Mbali na vifo vya watu hao wawili, ofisa huyo alisema hadi jana, kaya zaidi ya 100 hazikuwa na makazi na nyingi zimepoteza mali na vyakula.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dustan Kyobya alitaka wananchi wanaoishi maeneo hatarishi, wachukue tahadhari na kuondoka mara moja nyakati hizi za mvua kubwa inayonyesha maeneo mbalimbali ndani ya wilaya hiyo.

"Hiki ni kipindi cha msimu wa mvua, maji ni mengi, mvua inayonyesha ni kubwa tofauti na iliyotokea zamani,watu wanaokaa bondeni watoke na watoto tuwapeleke katika maeneo salama," alisema Kyobya.

Mkuu wa Wilaya Kyobya pia alielekeza wananchi kutoa taarifa kunapokuwa na changamoto zinazohusiana na mafuriko kwa kutumia viongozi wa kamati za maafa kuanzia ngazi za kitongoji, kijiji, kata, halmashauri hadi wilaya.

"Kamati hizi za maafa zikae na kufanya tathmini pale ambapo kuna changamoto na maeneo yeye mzunguko mkubwa wa maji kwenye taasisi za shule, watoto wasiende shuleni ili kuhakikisha wanakuwa salama," alisisitiza Kyobya.

Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo wakazi wake wameathiriwa na mvua kubwa zilizotabiriwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchjini (TMA) kwamba ingenyesha msimu huu.



Mwenyekiti wa mfuko wa Rehmat-fi-Sabililah Trust of Zanzibar, Hajat Yasmin Alloo (kulia), akikabidhi zawadi na cheti kwa mtoto Firdaus Abdulrahman Amour ikiwa ni pongezi kwa kufunga na kusali mwezi mtukufu wa Ramadhan, mjini Zanzibar jana, ambapo zaidi ya watoto 600 wa Unguja na Pemba wamezawadiwa na mfuko huo. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Dk. Mwinyi aongoza dua kumuombea Hayati Abeid Karume

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amejumuika na viongozi na wananchi mbalimbali katika dua maalum ya kumuombea Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume.

Dua hiyo ilifanyika katika ofisi kuu za CCM Kisiwandui sehemu ambayo mwili wake ulizikwa.

Katika dua hiyo ya kisomo cha hitma iliyofanyika jana ilianza na dua iliyosomwa na Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Hassan Ngwali, kisha kisomo cha hitma kikasomwa na Shekhe Abdulrahman Dedes na kuhitimishwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Kabi.

Dua hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kiserikali, kisiasa, dini na vyombo vya ulinzi na usalama akiwemo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah.

Wengine ni Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid.

Wengine ni viongozi wastaafu akiwemo Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Karume, Rais Mstaafu Dk. Ali Mohammed Shein, Waziri Kiongozi Mstaafu, Shamsi Vuai Nahodha, Makamu wa Pili Mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi.

Baadaya ya dua hiyo, baadhi ya viongozi na wanafamilia walipata fursa ya kuweka mashada ya maua katika kaburi la kiongozi huyo wa Zanzibar ambaye alifariki April 7 mwaka 1972.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya dua hiyo viongozi na wananchi waliohudhuria walisema alama kubwa aliyoiacha Mzee Karume itaendelezwa kwasababu ndiyo mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na kuikomboa Zanzibar.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif alisema Mzee Karume hatasahaulika kutokana na maendeleo mengi aliyoyafanya ikiwemo kuunganisha umoja wa wananchi wa Zanzibar katika kushikamana.

"Ukiachana na maendeleo makubwa ikiwemo ya miundombinu, afya, elimu, makazi, maji kwa kweli Wazanzibari hatutomsahau kiongozi wetu huyu ambae leo ametimizam miaka 52 tangu alipofariki" alisema Sharif.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema Mzee Karume akimsoma katika vitabu na kupata simulizi kutoka kwa wazazi kuwa ni mfano mzuri katika waasisi wa nchi, hivyo vijana wanapaswa kujifunza kutokana na msingi ya kiongozi huyo ikiwemo uzalendo na uwadilifu.

Mstahiki Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Muhammed Mussa, alisema Zanzibar imeingia katika kumbukumbu ya kumuenzi mwazilishi wa Mapinduzi ya Zanzibar na kuna mambo mengi ya kujifunza katika kifo chake, ikiwemo ulinzi na usalama katika nchi na maendeleo yanayoendelea.

Alisema kuna umuhimu wa kuwatunza na kuwaenzi wajane wa wanamapinduzi kwa sababu nao wanamchango mkubwa katika nchi, hasa kwa kipindi chote walichoishi na wanaume zao ambao ndiyo majemedari wa Mapinduzi ya Zanzibar.

# Nchimbi: Viongozi wote waombewe kutimiza wajibu

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema viongozi wote wakiwamo wa kitaifa na vyama vyote vya siasa wanapaswa kuombewa na viongozi wa dini ili wajue kwamba wote wana wajibu kwa nchi yao.

Balozi Dk. Nchimbi amesema kuacha kuwaombea baadhi ya viongozi katika makundi hayo au kuchagua wa kuwaombea na kuacha wengine, litakaloumia ni taifa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa hafla ya kufuturisha watoto yatima pamoja na dua kwa Rais Samia Suluhu Hassan, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama hicho (UVCCM), jijini Dar es Salaam.

"Tunashukuru sana kwa mapenzi makubwa ambayo mmeonyesha katika tukio la leo, kufuturisha kundi hili la watoto yatima na dua kwa Rais wetu, lakini naomba katika maombi yenu, tuwaombee viongozi wote wa Tanzania, viongozi wa serikali, CCM, vyama vya siasa vingine ili wajue kwamba kila mmoja ana wajibu kwa nchi yao," alisema.

"Ni wazi kwamba tukiacha kuwaombea baadhi ya viongozi, tukichagua kuwaombea na kuwaacha wengine...anayeumia ni taifa letu, kwa hiyo tuwaombee viongozi wote, watambue, wajue umuhimu wa kazi wanazozifanya kwa nchi yao, wajue umuhimu wa kuitumikia nchi yetu kwa uaminifu na waipende nchi yao, nawaomba msichoke...msichoke...msichoke kuliombea taifa letu."

Alisema ni wakati mwafaka kwa Watanzania kuendelea kumuombea dua Rais Samia Suluhu Hassan kwa uzalendo na kazi kubwa anazoendelea kufanya kwa taifa.

"Ni wakati mwafaka wa kumuomba Mungu atusaidie na apokee dua zetu na tunaweza kusema bila kigugumizi kwamba Rais Samia, anafanya kazi kubwa sana na kwa uzalendo wa hali ya juu, ana mapenzi ya kipee kwa Watanzania. Tunayo kila sababu ya kumuomba Mungu, amjalie hekima na nguvu zaidi na arefushe zaidi maisha yake ili aweze kuendelea kulitumikia taifa hili," alisema Balozi Dk. Nchimbi.

Pia, alipongeza kazi inayofanywa na viongozi wa dini ya kuwalea vijana kiimani.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya kuwalea vijana na kuwafundisha imani, na kadri mnavyowalea katika imani ndivyo watakavyokuwa viongozi bora kwa nchi yetu, kwa hiyo niendelee kusisitiza kwamba muendelee kufanya kazi hiyo ili tuwe na taifa lenye vijana wenye kujitambua na kuelewa wajibu wao kwa nchi yetu," alisena Balozi Dk. Nchimbi.

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Kawaida, alisema pamoja na mambo mengine, jumuiya hiyo inatambua umuhimu wa vijana kuwa na kipaumbele kwenye misingi ya imani.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi Kata ya Ilala, Sabry Sharif (kulia), akiongoza kampeni ya upandaji miti katika mitaa ya kata hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Jumuiya ya Wazazi Taifa. **PICHA: PILLY KIGOME**

# Wanaodaiwa kumshambulia Ofisa kilimo wafikishwa mahakamani

**Na Steven William,** MUHEZA

WATUHUMIWA wanane wakazi wa kata ya Kwezitu wilayani Muheza, wanaodaiwa kumjeruhi kwa kumpiga Ofisa Kilimo Kata ya Tongwe, Subira Mmbago wamefikishwa mahakamani.

Watuhumiwa hao wamesomewa mashtaka yao mwishoni mwa wiki Mahakama ya Hakimu Mkazi, Wilaya ya Muheza Tanga.

Watuhumiwa waliosomewa mashtaka ni Betwer Mtulo, Neema Mohamed, Emanuel Chaheza, Ernest Singa, Juma Joseph, Shabilu Rashid, Ramadhani Bakari na Juma Bikaila.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi Mahakama ya Wilaya ya Muheza, Joseph Njama kwa kushirikiana na Michael Msangawale, waliwasomea mashataka yao mbele ya hakimu wa mahakama hiyo Godfrey Haule.

Mwendesha mashtaka Njama alidai kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa katika kijiji cha Kambai, Kata ya Kwezitu kwa kumpiga na kumjeruhi Ofisa kilimo huyo ambaye ni msimamizi wa shamba la mwekezaji.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita katika kijiji cha Kambai kilichopo kata ya Kwezitu, wilayani Muheza.

Ilidaiwa kuwa wananchi hao walimjeruhi Ofisa kilimo huyo na kuchoma moto gari lake aina ya Suzuki wakimtuhumu kushindwa kusimamia maslahi yao na kusababisha wawekezaji kupewa eneo la zaidi ya ekari 500 bila tathmini ya kina kufanyika.

# Tanesco yatoa hadhari wananchi Kibiti, Rufiji

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme (Tanesco), limewataka wananchi wa Wilaya za Kibiti na Rufiji Mkoa wa Pwani, kuendelea kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara wakati shirika linaendelea kupunguza maji katika bwawa la Mwalimu Nyerere JNHPP.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Tanesco Kanda ya Mashariki, Mhandisi Kenneth Boymanda, wakati viongozi wa shirika hilo walipotembelea kukagua, kujionea na kufanya tathmini ya athari mbalimbali zilizojitokeza kutokana na mafuriko yaliyotokea.

Alisema ujenzi wa bwawa la JNHPP umesaidia kupunguza athari za mafuriko na katika maeneo hayo mara ya mwisho kutokea mafuriko ilikuwa mwaka 2021 na kwa sasa lina uwezo mkubwa wa kuhifadhi maji yaliyosaidia wananchi kutopata mafuriko kama ilivyokuwa.

"Shirika linaendelea kutoa tahadhari kwa wakazi wote wanaoishi kwenye ukanda wa chini wa Wilaya za Rufiji na Kibiti kuhusu ongezeko la maji. Ni vyema wananchi hasa wale wanaoishi kwenye maeneo ambayo mara zote yamekuwa yakikumbwa na mafuriko wachukue tahadhari ili kuokoa mali zao na uhai wao na pasitokee majanga makubwa ambayo yanaweza kuzuilika," alisema Boymanda.

Naye Mhandisi wa Maji kutoka JNHPP, Dismas Mbote alisema licha ya kuanza kutoa elimu ya kutosha kabla ya kufungulia maji bado timu ya wafanyakazi wa mradi wa JNHPP inaendelea kupiga kambi maeneo hayo kuhakikisha wananchi wanaondoka salama maeneo hatarishi.

"Tuko huku kujibu maswali ya wananchi, kutoa ufafanuzi na kurekebisha maneno ambayo kuna watu wasio na nia njema wanapotosha ukweli na kutaka kuigombanisha Serikali na wananchi. Sisi tunawaelimisha na kuwapa ukweli na wananchi wengi wanatuelewa na wao wanakiri kwamba mafuriko haya yamekuwepo kwa miaka mingi na yamekuwa yakija na kupita," alisema Mbote.

Kazi ya kupunguza maji katika bwawa la JNHPP lilianza rasmi Machi 8, 2024 na bado linaendelea kadri kina cha maji kinavyoonekana kuzidi huku likiendelea kupunguza kiasi cha maji yaliyopaswa kwenda kwa wananchi katika Wilaya ya Rufiji na Kibiti.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Edward Gowelle, alisema mradi wa JNHPP umepunguza kwa kiasi kikubwa mafuriko yaliyokuwa yakitokea katika Wilaya hiyo miaka ya nyuma.

Gowelle alisema kujengwa kwa JNHPP kumesaidia kujua kiwango cha maji kinachotolewa kwenda kwa wananchi na hivyo kufanya athari kuwa ndogo ikilinganishwa na namna ilivyokuwa wakati bwawa halijajengwa ambapo mafuriko yalikuwa yanatokea bila kujua kiwango cha mtiririko wa maji.

"Miaka hiyo ya nyuma kulikuwa hakuna tahadhari. Wananchi walikuwa wakishtukia tu maji yamejaa katika nyumba zao na mashamba yao. Kipindi hiki sisi serikali tulipata tahadhari mapema kutoka Tanesco kwa hiyo tulifikisha taarifa kwa wananchi ambao walichukua tahadhari kujinusuru na ndiyo sababu mpaka sasa hakuna kifo hata kimoja kilichoripotiwa kutokea kutokana na maji haya," alisema Gowelle.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Abdul Bakari Chobo, alisema Wilaya ya Rufiji imekuwa ikipata mafuriko mara kwa mara tangu yeye akiwa mdogo lakini ujenzi wa JNHPP umepunguza kwa kiwango kikubwa mafuriko kwani kwa miaka ya karibuni hawakuwahi kupata mafuriko.

"Mvua nyingi zinaendelea kunyesha kwenye ukanda wa nyanda za juu kusini na maji yamekuwa mengi kwa hiyo bwawa hili lisingekuwepo huenda madhara yangekuwa makubwa zaidi nawasihi watu kuacha upotoshaji wa taarifa kuwa sababu kubwa ya mafuriko ni ujenzi wa bwawa," alisema.

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# CRDB yapokewa kwa kishindo DRC

**LUBUMBASHI,** DRC

BENKI ya CRDB imepokewa kwa kishindo katika soko la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ikishuhudia kuvutiwa kwa kiasi kikubwa kwa wenyeji wa nchi hiyo.

Tangu kufungua milango yake ya kutoa huduma katikati ya mwezi Julai 2023 huko Lubumbashi, maelfu ya raia wa Congo na jumuiya ya biashara wamejitokeza kujiunga na benki hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Congo, Dk. Fred Msemwa, alibainisha mwishoni mwa wiki mafanikio hayo alipowasilisha ripoti katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wanahisa wa Benki hiyo.

Dk. Msemwa alisema mapokezi makubwa ambayo benki imeyapata ni ushahidi wa dhamira yao ya kutoa huduma na bidhaa bunifu za kifedha zinazoendana na mahitahi halisi ya watu wa Congo na biashara nchini humo.

"Ninafurahi kuwajulisha kuwa benki yetu ya CRDB Congo imepokewa vizuri na idadi kubwa ya watu wa Congo.

"Kujitokeza kwa wingi kwa wateja kunadhihirisha imani walioweka katika benki yetu. Tumejitolea kuhudumia wateja wetu kwa ufanisi na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya DRC," aliongeza.

Licha ya changamoto zilizokabili soko la Congo katika mwaka wa fedha wa 2023, ikiwamo mivutano ya kisiasa kutokana na uchaguzi, mfumuko wa bei pamoja na za kidunia ikiwamo vita vya Urusi na Ukraine, Dk. Msemwa alisema CRDB Congo imeanza vizuri katika soko hilo, ikiweka msingi imara wa ukuaji.

Alibainisha kuwa kwa miezi mitano ya uendeshaji hadi Desemba 2023, benki hiyo ilirekodi jumla ya amana ya wateja zenye thamani ya Faranga za Congo (CDF) bilioni 2.5, na jumla ya mali zenye thamani ya Faranga za Congo (CDF) bilioni 126.

Akizungumzia mafanikio ya kuvutia ndani ya muda mfupi wa uendeshaji nchini humo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alibainisha kuwa CRDB Congo imeanzisha huduma ya malipo kuvuka mipaka iliyopewa jina la 'CRDB Umoja'.

Alisema ubunifu huo umesaidia kuboresha huduma za malipo kwa watu, kampuni na taasisi zinazofanya biasharaa kati ya Tanzania, Congo, na Burundi.

"Kwa Kiasi kikubwa hii imesaidia kuchochea ukuaji wa biashara katika nchi za ukanda huu wa Afrika ya Mashariki.

"Kwa Watanzania wanaofanya biashara kwenda DRC, niwahakikishie kuwa Benki ya CRDB iko tayari kufanikisha miamala yao ya kifedha kwa urahisi na uharaka pamoja na kuwapatia huduma nyingine za uwezeshaji zitakazosaidia kukuza biashara zao," alisema.

Nsekela pia alishukuru Rais wa DRC, Felix Tsishekedi na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri kwa ushirikiano wa biashara, ambayo yamekuwa msukumo wa kuingia kwa benki hiyo Congo na kupelekea mwanzo mzuri katika nchi hiyo.

Dk. Ally Laay, Mwenyekiti wa Bodi ya Kundi la Benki ya CRDB, alieleza matumaini yake kuhusu mwanzo wa mzuri wa kampuni hiyo tanzu ya CRDB Congo na namna inavyoendana na azma, dira na mkakati mpana wa benki hiyo katika kuyafikia masoko mengi barani Afrika.

Alisema, "Mwanzo mzuri wa CRDB Bank Congo si tu unachangia lengo letu la kuwa benki inayoongoza Afrika, lakini pia unachangia katika azma yetu ya kuboresha maisha na uchumi wa bara hili," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Congo, Jessica Nyachiro alisisitiza uwezekano mkubwa wa benki hiyo kuchangia kasi ya ukuaji uchumi wa ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati.

Jessica alisema mpango wa benki hiyo ni kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika miundombinu ya kidijitali, jambo litakaloboresha jinsi watu na biashara nchini Congo wanavyoendesha shughuli zao za kibenki.

Alisema benki hiyo inalenga kuimarisha zaidi nafasi yake katika soko la Congo kwa kupanua huduma zake katika maeneo mengine ya Lubumbashi, Kinshasa, Kivu Kaskazini na Kusini, Bukavu na maeneo mengine muhimu.

Benki ya CRDB Congo imeanzishwa kwa ushirikiano wa Benki ya CRDB PLC, Taasisi ya Fedha ya Maendeleo ya Norway (Nor-Fund) na Shirika la Uwekezaji la Denmark kwa ajili ya nchi zinazoendelea (IFU).

Benki hiyo kwa sasa inatoa huduma zake nchini Congo kupitia tawi lake la Hyponese lililoko barabara Mama Yemo huko Lubumbashi pamoja na ATM zilizoko katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

## Vyuo vikuu Norway vyaikumbuka Shule ya Uhuru Mchanganyiko

**Na Grace Mwakalinga,** Dar es Salaam

VYUO vikuu vya Norway vimetoa msaada wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati kukabidhi vifaa hivyo, Prof. Bente Dale Malones wa Chuo Kikuu cha Molde, Norway, alisema vifaa hivyo vitapunguza tatizo la uhaba wa nyenzo za kufundishia, kujifunzia na vifaa vya michezo shuleni huko; vinamegharimu Sh. milioni 9.5.

Alisema shule hiyo ambayo ni ya mfano kutembelewa, imekuwa na mambo mengi mazuri ya kujifunza kama vile uwezo wa watoto hao darasani na ari ya walimu kufundisha, kitu kinachopaswa kuigwa.

Alianisha vifaa walivyotoa ni madaftari, kalamu za wino na risasi, viti mwendo, vifaa vya usafi, mipira, sabuni, maandishi ya nukta nundu, midoli, ndoo za kuhifadhia maji na vifaa vingine.

Akipokea msaada huo, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Hajrati Kashakara, alisema vitasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa hivyo kwa watoto hao, akiomba ushirikiano huo uendelee ili wapate vitu vingi kwa ajili kuwasaidia kusoma katika mazingira mazuri.



Rais wa Rwanda, Paul Kagame akiwa katikati ya wanajeshi wakati wa kushiriki kumbukizi ya mauaji ya kimbari yaliyotokea mwaka 1994 nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

## Rwanda yaadhimisha miaka 30 mauaji kimbari

**KIGALI,** Rwanda

TAIFA la Rwanda limeadhimisha miaka 30 tangu yafanyike mauaji ya kimbari dhidi ya jamii ya Watutsi na Wahutu, ambayo yalichukua uhai wa watu takribani 800,000 ikiwa ni tukio baya zaidi la mauaji ya karne ya 20 yaliyowahi kushuhudiwa katika bara la Afrika.

Wakati wa maadhimisho hayo yaliyofanyika jana Rais wa Rwanda Paul Kagame, aliwasha mwenge ikiwa ni ishara ya kuwakumbuka wahanga wa mauaji hayo kwenye eneo la kumbukumbu ya mauaji ya kimbari katika mji wa Kigali.

Mauaji hayo yalitokea Aprili 7 mwaka 1994 na kwamba zaidi ya wahanga 250,000 wanaaminika walizikwa katika eneo hilo la kumbukumbu.

Bendi ya jeshi ilipiga nyimbo za huzuni, wakati Rais Kagame alipoweka mashada ya maua kwenye makaburi ya halaiki, akiwa amezungukwa na viongozi wa kigeni wakiwemo wakuu kadhaa wa nchi za Afrika na aliyekuwa Rais wa Marekani wakati wa mauaji hayo Bill Clinton.

Clinton, alisema kushindwa kuepusha mauji hayo ya halaiki nchini Rwanda ni kosa kubwa lililofanywa na utawala wake.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron katika ujumbe wake alisema Ufaransa na washirika wake wa Magharibi na wa Afrika wangeliweza kuyazuwia mauaji hayo lakini hawakuwa na nia ya kufanya hivyo.

Mwanadiplomasia wa zamani wa Jamhuri ya Czech, Karel Kovanda, aliyekuwa Balozi wa kwanza wa Umoja wa Mataifa kutamka hadharani matukio ya mwaka 1994 kuwa ni mauaji ya halaiki, karibu mwezi mmoja baada ya mauaji hayo kuanza, alisema mauaji hayo si jambo la kusahaulika.

Kumbukumbu hiyo ya Rwanda inakumbushia kipindi cha kutisha katika taifa hilo la Afrika Mashariki ambako jamii ya Wahutu wenye msimamo mkali walifanya mauaji ya halaiki yaliyosababisha umwagikaji damu nchini Rwanda.

Umoja wa Mataifa unasema karibu watu 800,000 waliuawa nchini Rwanda. Na kwamba hadi leo, makaburi ya halaiki yanaendelea kugundulika katika nchi hiyo yenye watu karibu milioni 14.

Ilielezwa kuwa mauaji ya Rais Juvenal Habyarimana wa kabila la Hutu Aprili 6, baada ya ndege yake kudunguliwa katika anga ya Rwanda, yalichochea Wahutu wenye msimamo mkali na wanamgambo wa 'Interahamwe' kufanya mashambulizi, yaliyosababisha wahanga kuuawa kwa risasi, kupigwa vibaya na wengine kuchinjwa. **DW**

# COASTAL YAMKINGIA KIFUA KOCHA

Na Saada Akida

UONGOZI wa Coastal Union umesema haujamwekea mtego wowote Kocha Mkuu wa timu hiyo raia wa Kenya, David Ouma, ikiwamo wa kupoteza mechi ili kumfuta kazi ya kukinoa kikosi hicho.

Kauli hiyo imekuja baada ya taarifa kuzagaa kuwa viongozi hao wamempa mechi moja na kama akipoteza anafungashiwa virago vyake huku akitajwa aliyekuwa Kocha wa Tabora United, Goran Kopunovic, anatarajiwa kubeba mikoba yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Coastal Union, Abass Elsabri, alisema hakuna ukweli wowote juu ya kutaka kumuondoka wala kumpa mtihani wa kushinda baadhi ya mechi.

**Alisema ataendelea kukinoa kikosi cha timu hiyo kulingana na mkataba wake wa miaka miwili utakapofikia tamati kwa sababu amefanikiwa kuitoa timu kutoka nafasi ya 14 hadi 4.**

"Hayo mambo yanatengeneza kutuondoa katika mstari kwa sababu kuna taarifa kuwa baadhi ya wachezaji wetu kuhusishwa na klabu kongwe hapa nchini, lakini pia kuna hilo jambo la kocha Ouma kuachana naye.

"Mashabiki wetu wanatakiwa kupuuza hizo tetesi na kushikamana kuwa wamoja, hakuna ukweli juu ya kutaka kumfukuza kocha wetu wala kumpangia mechi kuwa asiposhinda tutamuonda hilo halipo," alisema Abass.

Aliongeza kuwa kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika michezo iliyopo mbele yao ili kushinda na hatimaye kubaki kwenye nafasi ya juu.

Coastal Union inashika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 30, wakishinda nane, sare sita na kupoteza michezo saba na sasa imefuzu kucheza robo fainali ya Kombe la CRBD Bank Federation.

TUMEREJEA...




Wachezaji wa Yanga baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere juzi wakitokea Afrika Kusini kwenye mechi ya marudiano ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns, ambayo mabingwa hao wa Tanzania walitolewa kwa mikwaju ya penalti 3-2 baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare tasa. NA MPIGAPICHA WETU

## Ashinda gari 'Benki ni Simbanking' ya CRDB

Na Mwandishi Wetu

Nickson Kiungo, mkazi wa jijini Dar es Salaam na mteja wa siku nyingi wa Benki ya CRDB, ameibuka mshindi wa kwanza wa gari aina ya Nissan Dualis katika Kampeni ya Benki ni Simbanking.

Akichezesha droo ya kumpata mshindi wa kwanza wa gari wa kampeni hiyo mwishoni mwa juma, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili, alisema Kiungo ameshinda gari hilo kutokana na miamala mingi aliyoifanya kupitia simu yake ya mkononi.

"Huyu ni mshindi wetu wa kwanza. Tunayo magari matatu yamebakia kwa ajili ya washindi watakaopatikana katika kampeni hii ya Benki ni Simbanking ambayo inatoa zawadi nyingine kama vile bajaji, bodaboda na simu za kisasa. Watanzania waendelee kutumia Simbanking ya Benki ya CRDB ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushinda zawadi tulizonazo," alisema Adili.

Adili alisema gari hilo limekatiwa bima kubwa na litajazwa mafuta kabla ya kumkabidhi mshindi ili aanze kulitumia bila kuhitaji kuingia gharama za ziada.

Ili kujiweka kwenye nafasi ya kujishindia zawadi zilizopo, Adili alisema mteja wa Benki ya CRDB anatakiwa kutumia huduma za Simbanking kama anatumia simu ndogo au kuingia kwenye programu yake inayopatikana kwa wenye simu kubwa ambayo aliitaja ni rahisi na ina ufanisi mkubwa.

Adili alisisitiza kuwa ni ngumu kuepuka uchumi wa kidijitali kwa sasa, hivyo Watanzania hawapaswi kubaki nyuma katika kutumia huduma za Simbanking, aliitaja ni jukwaa bora zaidi nchini na linaloongoza kwa kutumiwa kati ya programu za benki zilizopo.

Ikiwa benki kiongozi nchini, mkuu huyo alisema CRDB inahakikisha wakati wote inaboresha huduma zake ili kukidhi mahitaji ya wateja ikitambua kwamba matarajio yao yanabadilika kila siku.

Akizungumzia zawadi aliyoshinda, Kiungo alisema amekuwa anatumia huduma za Simbanking kwa muda mrefu, hivyo ni furaha kwake kuona miamala yake imetambulika kiasi cha kuzawadiwa na benki.

"Ni bahati iliyoje. Ninafahamu Benki ya CRDB ina wateja wengi, hivyo mimi kuibuka mshindi ni bahati. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii," alisema Kiungo.

Mbali na mshindi huyo wa gari, kwenye droo hiyo iliyochezeshwa mwishoni mwa wiki, washindi wengine wawili wa simu janja walipatikana. Washindi hao ni Daud Peres Manyama na James Alex Kiambati.

Katika kampeni hiyo kila mwezi hutoa bajaji moja na bodaboda mbili kwa wateja wanaofanya miamala mingi kupitia programu yake ya Simbanking inayohamasisha uchumi wa kidijitiali kwa kuwawezesha wananchi kufanya miamala mingi pasipo kutumia fedha taslimu.

## Zimamoto yaipania New King FA Cup

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto itawavaa Wafalme wa Kinyasini New King FC Aprili 21, mwaka huu, katika hatua ya 16-bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Kamati ya Mashindano ya ZFF mchezo huo utapigwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Katika mchezo huo wa hatua ya 16-bora Zimamoto imesema inaweza ikakutana na upinzani mkubwa kutoka kwa Wafalme wa Kinyasini hao, wanaotokea Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Timu hiyo ipo Ligi Daraja la Kwanza Kanda na imekuwa ikifanya vizuri katika michuano hiyo licha ya kutofika fainali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmed Hilali 'Tedi', alisema licha ya upinzani wanaotarajia kuupata, yeye anakiamini kikosi chake kinaweza kufanya vizuri kutokana na maandalizi ya mapema waliyofanya.

Alisema mchezo huo kwao wao ni mgumu kwakuwa wanawafahamu vizuri wapinzani wao katika Kombe la FA, hivyo lazima wawe makini ili kutimiza lengo lao la kusonga mbele.

Alisema kuvuka katika hatua 16-bora kutawasafishia njia katika kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi katika hatua inayofuata ya robo fainali.

"Si mchezo rahisi, lakini pia hautakuwa mgumu uwanjani iwapo wachezaji watacheza vizuri na kujua nini lengo letu katika mashindano haya,"alisema.

Hata hivyo, alisema maandalizi ya mapema waliyofanya ikiwamo kutovunja mazoezi katika mwezi huu wa Ramadhani, hiyo inaonesha kuwa wachezaji wao wanakiu ya kuhakikisha wanfanya vizuri katika hatua hiyo.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ALENGWA CITY

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kalvin Phillips, 28, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo West Ham, amepangwa kama mmoja wa walengwa wa Fulham msimu ujao. ***(Football Transfers)***

### RODRI KUONGEZEWA MSHIKO

KLABU ya Manchester City inataka kumzawadia Rodri, 27, kwa nyongeza ya mshahara ambayo itamfanya kiungo huyo wa kati wa Hispania abaki na klabu hiyo katika maisha yake yote ya soka. ***(Mirror)***

### GYOKERES AIVUTIA ARSENAL

ARSENAL na Chelsea zinavutiwa na Viktor Gyokeres, 25, lakini Sporting Lisbon hawatakubali chini ya euro milioni 100 kwa mshambuliaji huyo. ***(Pedro Sepulveda)***

### PEREIRA ATAKIWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid inavutiwa na kiungo wa kati wa Fulham raia wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### TEN HAG NA UNITED

BODI ya Manchester United itasubiri hadi mwishoni mwa msimu kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa kocha, Erik ten Hag, licha ya shinikizo kwenye nafasi ya Mholanzi huyo. ***(Times)***

### RAMSDALE KUONDOKA

GOLIKIPA wa England, Aaron Ramsdale,25, anatarajiwa kuondoka Arsenal msimu huu, huku mchezaji huyo akilengwa na Newcastle United. ***(Football Insider)***

### MOTTA KUMRITHI TEN HAG

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumteua Kocha wa Bologna, Thiago Motta, kama mbadala wa Erik Ten Hag. ***(Gazzetta dello Sport)***

### LAMPARD ATAJWA CANADA

KOCHA wa zamani wa Chelsea Frank Lampard, ameibuka kuwa mgombea wa kushtukiza kuchukua mikoba ya kuinoa Timu ya Taifa ya Canada. ***(Telegraph)***

### ALEXANDER-ARNOLD KIFUNGO

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo na Trent Alexander-Arnold, 25, kuhusu mkataba mpya wa beki huyo wa kulia wa England. ***(Football Insider)***

### MODRIC AWEKEWA TANGAZO

DINAMO Zagreb imelipa tangazo la ukurasa mzima katika gazeti la michezo la Marca, kwenye jaribio la kumshawishi kiungo wa kati wa Croatia, Luka Modric, 38, kurejea katika klabu yake ya kwanza iwapo ataamua kuondoka Real Madrid msimu huu. ***(ESPN)***

### MBAPPE ASITISHIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imesitisha mazungumzo ya kuongeza mkataba na mdogo wa Kylian Mbappe, Ethan, 17, huku mkataba wa sasa wa kiungo huyo wa kati wa Ufaransa ukimalizika Juni. ***(RMC Sport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA AWAJIBU WAKOSOAJI WAKE

**ROYADH,** Saudi Arabia

KARIM Benzema amewajibu wakosoaji wa uchezaji wake tangu alipohamia Klabu ya Al Ittihad ya Saudia, akisema anahitaji usaidizi na hawezi kushinda michezo peke yake.

**Mshindi huyo wa zamani wa tuzo ya Ballon d'Or alikua miongoni mwa majina mashuhuri kuhamia Saudi Arabia msimu uliopita wa majira ya joto baada ya kumaliza miaka 14 akiwa na Real Madrid.**

Hata hivyo, amefunga mabao tisa pekee katika mechi 20 za ligi katika msimu wake wa kwanza nchini Saudia. Al Ittihad, mabingwa wa msimu uliopita, wanashika nafasi ya nne katika msimamo, wakiwa na pointi 30 nyuma ya viongozi Al Hilal.

Alipoulizwa baada ya Al Ittihad kutoka suluhu na Al Taawoun Ijumaa kwa nini mashabiki walikuwa hawamuoni Benzema yule wa Real Madrid, aliiambia Action with Walid: "Kwa sababu si mchezo sawa, sio wachezaji sawa.

"Nahitaji msaada uwanjani, siwezi kushinda mchezo mmoja peke yangu. Nahitaji mchezaji mwingine, nahitaji vitu vingi. Lakini ni tofauti, ni msimu wangu wa kwanza Saudia. Natumai nitamaliza msimu vizuri, natumaini nitashinda.

Benzema mwenye umri wa miaka 36, alisaini mkataba wa miaka mitatu na Al Ittihad msimu uliopita wa majira ya joto wenye thamani ya euro milioni 400.

Lakini ESPN iliripoti kwamba Benzema aliangalia chaguzi nyingine kwenye dirisha la uhamisho wa Januari baada ya miezi sita ya kwanza ya Jeddah.

Mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa alijua kwamba Al Ittihad wangemruhusu kuondoka, lakini alifikiria kurejea Ulaya kama uwezekano.

Chelsea na klabu yake ya nyumbani Lyon wote waliuliza kuhusu upatikanaji wake, vyanzo viliiambia ESPN.

Benzema aliifungia Madrid mabao 354 katika mechi 648 huku akiweka rekodi ya kutwaa mataji 25, yakiwamo mataji manne ya LaLiga, matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, matatu ya Copa del Rey, manne ya Supercopa, manne ya UEFA Super na matano ya Klabu Bingwa Dunia.

> Nahitaji msaada uwanjani, siwezi kushinda mchezo pekeyangu, ni msimu wangu wa...

# LEVERKUSEN POINTI 3 KUBEBA BUNDESLIGA



Sport

**MUNICH,** Ujerumani

VINARA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayer Leverkusen walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Union Berlin, Jumamosi na kufikia rekodi ya kutopoteza katika mechi 28 mfululizo na wanakaribia kutwaa taji lao la kwanza la ligi wakiwa na faida ya pointi 16 kileleni na mechi sita zilizosalia.

Kikosi cha Xabi Alonso, ambacho hakijapoteza katika mechi 41 kwenye michuano yote msimu huu, kinaweza kutwaa taji lao la kwanza la Bundesliga na taji la kwanza baada ya miaka 31 kwa ushindi nyumbani dhidi ya Werder Bremen wiki ijayo.

Wako na pointi 76 huku wakiwa wamesalia na mechi sita na Bayern Munich wanaoshika nafasi ya pili wakiwa na pointi 60 kutokana na kichapo cha kushangaza cha mabao 3-2 kutoka kwa Heidenheim, ikiwa ni kupoteza kwao kwa pili mfululizo kwenye ligi.

"Ninajivunia sana timu. Tulijiandaa vema na tulikuwa na mawazo yanayofaa. Hali sasa ni nzuri sana kwetu na labda tutakuwa na kitu cha kusherehekea wiki ijayo," alisema Xabi Alonso akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini kabla ya wiki ijayo kuna Ligi ya Europa na hapo ndipo umakini ulipo sasa."

Leverkusen, ambayo imekuwa ikidhihakiwa kwa muda mrefu kama 'Neverkusen' kutokana na kukosa mataji katika miongo kadhaa iliyopita, wametinga fainali ya Kombe la Ujerumani.

Pia watamenyana na West Ham United wiki ijayo katika mechi yao ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Europa.

"Sipendi kufananishwa. Tuna namna yetu ya kufanya mambo na tumefanya hivyo tangu mwanzo na tumeendelea hivyo," alisema Alonso.

"Tunataka kuendelea kwa njia sawa bila kujali kama ni Ligi ya Europa au Kombe la Ujerumani."

Licha ya kupata nafasi nyingi, timu ya Alonso ililazimika kusubiri hadi dakika za lala salama za kipindi cha kwanza ndipo Florian Wirtz akafunga kwa penalti. Dakika za awali Union ilimsababishia Robin Gosens kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Union haikuwahi kurejea tena ikiwa na mchezaji chini kipindi cha pili na Leverkusen walihitaji tu kudhibiti mchezo, wakishikilia pointi tatu kwa urahisi ili kufikia rekodi ya ligi kwa mechi nyingi mfululizo za kutopoteza.

# *Man United yataja bei ya Sancho*



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ipo tayari kupokea zaidi ya euro milioni 40 ili kuachana na winga Jadon Sancho, kwa mujibu wa ripoti.

Sancho alijiunga na Borussia Dortmund kwa mkopo Januari baada ya kutofautiana na kocha Erik ten Hag, lakini mpango huo haujumuishi chaguo la uhamisho wa kudumu na hivyo winga huyo kwa sasa anatarajiwa kurejea Old Trafford msimu huu wa majira ya joto.

Hata hivyo, iwapo Erik ten Hag ataendelea kuinoa United, Sancho huenda akatafuta kuondoka kwa kudumu na Sky Sport inaeleza kuwa anataka kubaki na Dortmund, ambayo pia inataka kufanya makubaliano na United.

Kikwazo kikuu kwa Dortmund ni gharama yake, kwani United ililipa pauni milioni 73 kumsajili Sancho mwaka 2021, na hivyo kumsainisha mkataba mnono ambao unatarajiwa kumalizika msimu wa majira ya joto wa 2025, na wanatafuta karibu nusu ya kiasi hicho ili kumuuza Sancho.

Kutumia fedha za aina hiyo kwa mchezaji mmoja itakuwa ngumu sana kwa Dortmund, ambayo pia haiwezi kutoa popote karibu na aina sawa ya mshahara anayopokea Sancho kwa sasa.

Mkataba wa kudumu bado haujatolewa lakini mazungumzo kati ya Dortmund na United bado yako mbali sana na azimio hilo.

Sancho amefunga mabao mawili na pasi mbili za mabao katika mechi 11 alizocheza hadi sasa akiwa na Dortmund, ambapo viongozi wa klabu hiyo wamekiri wazi kuwa hawakutarajia mengi kutoka kwa mchezaji huyo ambaye alikaa nje ya uwanja kwa miezi minne kabla ya kujiunga nao.

Mustakabali wa Sancho unaweza kuunganishwa na winga mwingine wa Dortmund, Donyell Malen.

Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa katika kiwango bora na akiwa amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake, anaaminika kuwa na nia ya kuhamia Ligi Kuu England.

## Felix amefichua Silva kuitaka Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

JOAO Felix amefichua kuwa mchezaji mwenzake wa Ureno, Bernardo Silva ameonesha nia ya kutaka kusajiliwa Barcelona.

Huku kukiwa na tetesi za uhamisho zinazomhusisha Silva na uwezekano wa kuhamia Katalunya, uidhinishaji wa Felix unaongeza uzito mkubwa katika hali hiyo.

Ripoti kutoka Hispania zimedai kuwa Silva ana nia ya kutaka kujiunga na Barca, na hivyo kuchochea tetesi kali zinazomhusu nyota huyo wa Ureno.

Akizungumza na Jijantes FC, Felix alisema angependa Silva ajiunge naye Barcelona na wawili hao wamezungumza kuhusu matarajio kama hayo.

"Kama ningekuwa Deco (Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona), kwa siku, ningemsajili Bernardo Silva bila shaka," alisema Felix.

"Acha wamlete. Umemuona akicheza? Ni bora zaidi kama mtu. Anatoka kizazi cha Joao Cancelo. Sasa wachezaji wanadumu hadi wana miaka 35 mpaka 36.

"Shemeji yake yuko hapa. aliniuliza kuhusu jinsi mambo yalivyo hapa, hali ya hewa, masuala ya kodi...nilimwambia ni sawa kwake kuja.

"Sidhani kama Manchester City itafanya iwe rahisi."

Felix pia alifichua kwamba Silva angetamani kuvaa jezi ya kifahari akiwa Barca - jezi iliyowahi kupambwa na gwiji wa klabu hiyo,Lionel Messi.

"Angependa kuvaa namba 10," aliongeza Felix.

"Ni namba muhimu sana kwenye klabu, huwezi kumpa mtu yeyote tu, unapaswa kuwa makini. Ni namba ninayoipenda sana, lakini sijawahi kuivaa."



## Benchikha aweka wazi wakusajiliwa

INATOKA UKURASA 24

tupambane na kuwekeza kwa kupata watu wa kutupeleka huko.

"Tupo katika mchakato huu wa kuwekeza kwa kuleta watu wenye uzoefu wa kucheza nusu fainali kuja kuungana na waliopo sasa kupigania timu kufika hatua hiyo ambayo Wanasimba wanaiota," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa wanafanya kazi kubwa kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwenye michezo yote miwili na kujiandaa kwa msimu ujao.

"Al Ahly, Mabingwa watetezi wa michuano hii, ndio timu ya Karne ya Afrika na pia kinara wa kuchukua mara nyingi taji hili kwa hiyo kutolewa nao si jambo la kusema tutakaa na kuanza kujilaumu," alisema Meneja huyo.

Kwa upande wa beki wa Kimataifa wa Simba, Che Fondoh Malone, alisema ameumia sana kwa timu yake kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini hawana jinsi wanasahau yote na sasa kujiandaa na michezo iliyopo mbele yao.

Alisema wanatakiwa kujipanga kwa ajili ya mashindano mengi kuhakikisha wanafanya vizuri na kuipambania heshima ya nembo ya Simba katika michuano mingine ikiwamo Ligi Kuu na Kombe la CRBD Bank Federation .

Che Malone alisema hakuna mchezaji ambaye atafurahishwa na matokeo waliyoyapata nchini Misri na anaimani ni mpira na sasa wanajipanga kwa michezo ijayo.

"Tunasahau mchezo uliopita na sasa tunaangalia kilichopo mbele yetu, imeuma lakini hatuwezi kuendelea kuwaza kilichopata na tunahitaji kufanya vizuri kwenye michezo iliyopo mbele yetu na kusonga mbele," alisema beki huyo.

Kikosi cha Simba kimeondoka jana kuelekea Kigoma tayari kwa mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la CRDB Federation dhidi ya Mashujaa FC utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Lake Tanganyika.

## Gamondi mguu nje ndani Yanga

INATOKA UKURASA 24

Ligi Kuu wamepatiwa taarifa zote zinazohusiana na mchezo huo na maandalizi yake yanaanza mara moja ili hakikisha unafanyika katika kiwango cha juu kinachoendana na michezo mikubwa ya ligi ya sita kwa ubora Afrika," ilieleza taarifa hiyo iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi nchini, TPLB.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye uwanja huo, Novemba 5, mwaka jana, Simba ikiwa mwenyeji, ilikutana na kipigo cha mabao 5-1.

# COASTAL, PRISONS, MASHUJAA FC ZAANZISHA TIMU ZA WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU za Coastal Union, Mashujaa FC na Prisons, zimeanzisha timu za mpira wa miguu kwa wanawake katika kile kinachoelezwa kuwa ni matakwa ya kikanuni ya leseni za klabu siku za usoni.

**Kuanzishwa kwa timu hizo kunafanya timu za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo pia zina vikosi vya soka la wanawake kufikia nane.**

Klabu ya Coastal, imeanzisha timu yake inayoitwa Coastal Ladies ambayo kwa sasa inashiriki Ligi ya Mkoa wa Tanga ambapo wikiendi hii ilitoa kipigo cha mabao 24-0 dhidi ya Mwambao Gold, mechi ikichezwa, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Matarajio yetu ni kupanda hadi Ligi Kuu ili kwenda kutoa ushindani dhidi yaa timu kubwa za huko," alisema Abass El Sabri ambaye ni Ofisa Habari wa Klabu ya Coastal Union.

Klabu ya Mashujaa FC imetangaza kuichukua timu ya Amani Queens iliyoshuka daraja msimu uliopita na sasa itajulikana kama Mashujaa Queens.

Timu hiyo itashiriki Ligi Daraja la Pili msimu huu, ikiwa kwenye mkakati wa kurejea Ligi Kuu ya Wanawake msimu ujao.

Klabu ya Prisons inayomilikiwa na Jeshi la Magereza nayo imeanzisha timu ya soka wanawake, Prisons Queens ambayo kwa sasa ipo kambini ikijiandaa kushiriki Ligi ya Wanawake Mkoa wa Mbeya.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza timu hiyo iko chini ya Kocha Mkuu, Roland Malambi, na lengo ni kuthamini na kukuza vipaji vya soka kwa akina dada.

"Malengo yetu kwa sasa ni kupandisha timu Ligi Kuu na baadaye kuchukua ubingwa," ilisema taarifa hiyo.

Kabla ya timu hizo tatu kuwa na timu za wanawake, timu za Ligi Kuu ambazo zilikuwa na vikosi vya wanawake ni Geita Gold Queens, JKT Queens, Yanga Princess, Simba Queens, na Baobab Queens ambayo inamilikiwa kwa ubia na Azam FC.

Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF, Salum Madadi, wakati akiwa Mkurugenzi wa Mashindano, alisema baada ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (CAF), kuzitaka timu zote zinazocheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kuwa na timu za wanawake, TFF nayo misimu michache baadaye itakuja na kanuni hiyo ya kuzitaka timu zinazocheza Ligi Kuu kuwa na timu za wanawake.

**PATASHIKA...**




Beki wa kushoto wa Brighton & Hove Albion, Pervis Estupinan, akihaha kumdhibiti winga wa Arsenal, Bukayo Saka, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Falmer juzi na Arsenal kushinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Jamburi matumaini kibao kubaki Ligi Kuu*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU ikiendelea kuhaha kubaki Ligi Kuu Zanzibar kwa kumaliza nafasi za juu msimu huu, timu ya Jamburi imesema mpango wao huo utaimarishwa zaidi kwa kuwa wanaamini katika michezo 10 iliyosalia iwatoa walipo kwa sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana Kocha Msaidizi wa timu ya Jamhuri, Mfaume Shaaban, alisema wanasuka mipango imara ili kuhakikisha wanacheza tena Ligi Kuu msimu ujao. Jamhuri ambayo makazi yake yapo Wete Pemba, ni miongoni mwa timu ambazo zipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzinibar wenye timu 16, ligi ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Kocha huyo alisema hesabu na mipango yao wanaielekeza katika michezo 10 iliyobaki kwa kuhakikisha wanapata alama za kuwaondoa katika hatari ya kushuka daraja.

Alisema timu hiyo licha ya kuvunja mazoezi kupisha mwezi wa Ramadhani, hiyo haitawazui kutimiza lengo na mikakati yao ushindi katika michezo iliyosalia.

Alisema miongoni mwa mpango mkubwa ni kuhakikisha hawapotezi kwa kufungwa katika michezo yote watakayocheza ugenini (Unguja), lakini pia kupata alama tatu kwa michezo yote watakayocheza nyumbani Kisiwani Pemba.

Aidha, alisema timu hiyo inatarajia kuanza mazoezi mapema mwezi Eid pili, ili kuajiandaa na michezo 10 ya lala salama katika ligi hiyo ambayo inatarajiwa kuongezeka ushindani.

Timu ya Jamhuri ipo nafasi ya 15 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 18, baada ya kushuka dimbani mara 20, ambapo imeshinda michezo minne, sare sita na kupoteza mechi 10.

Michezo
Jumatatu Aprili 8, 2024
Nipashe



Benzema awajibu wakosoaji UKURASA 22

# Gamondi mguu nje ndani Yanga

**Na Adam Fungamwango**

## Kuiongoza Yanga kuivaa Simba Aprili 20, huku akieleza hana ukakika...

HUKU mashabiki na wanachama wa Yanga wakifurahia namna timu yao ilivyocheza vizuri michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikifika hatua ya makundi baada ya miaka 25, lakini pia ikitinga robo fainali kwa mara ya kwanza, kocha aliyefanya kazi hiyo, Miguel Gamondi, amesema hana uhakika wa kuendelea kubaki katika klabu hiyo kwa msimu ujao.

**Gamondi, ambaye ni kocha mkuu wa timu hiyo, alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam baada ya kuwasili wakitokea Afrika Kusini ambapo walitolewa na Mamelodi Sundowns kwa mikwaju ya penalti 3-2 kutokana na dakika 90 za pili kumalizika kwa suluhu kama zile za awali katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Alipoulizwa kuhusu mipango yake ya msimu ujao baada ya kuichukua Yanga msimu wa kwanza na kuiingiza makundi baada ya miaka 25 kupita, huku akiifikisha robo fainali kwa mara ya kwanza tangu mfumo mpya wa michuano hiyo kuendeshwa kwa mtindo wa ligi ulipoanzishwa mwaka 1997, Gamondi alikataa kuelezea kwa madai hana uhakika wa kuendelea kuwapo na ataelezea kama atakuwapo kipindi hicho.

“Siwezi kuelezea hilo kwa sababu sina uhakika kama nitakuwapo kwa hivyo siwezi kuelezea mipango yoyote ya baadaye,” alisema.

Lakini kuhusu mbinu alizotumia kuweza kuisumbua Mamelodi inayosifika kwa kucheza soka la kuvutia Afrika, alisema ana furaha kubwa kwa kiwango walichoonyesha, akiwapongeza wachezaji wake kwa kucheza kwa maelekezo yake na kwa usahihi zaidi, wakiongeza na juhudi, upambanaji na kujituma.

“Nina furaha kwa kiwango tulichocheza na pia uwezo wa wachezaji wangu, walichofanya ni kucheza kwa maelekezo na kwa usahihi, kujituma, nidhamu na kupambana, usisahau tulikuwa tunacheza na Mamelodi Sundowns. Tulizuia mianya yao yote ambayo walikuwa wanatumia ili kufanya mashambulizi, wametengeneza nafasi chache sana za kufunga kitu ambacho si kawaida, hii si sifa kwa Yanga tu bali ni kwa Tanzania nzima,” alisema Gamondi.



Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi

Kocha huyo alikiri kuwa si kazi rahisi kucheza na timu hiyo kwani kila mtu anafahamu kuwa ni moja kati ya timu kubwa barani Afrika, huku pia akikumbushia bao walilonyimwa.

Katika hatua nyingine ya mzunguko wa pili ya watani wa jadi, Simba na Yanga imepangwa kuchezwa Aprili 20, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, imeeleza kuwa mchezo huo namba 180, awali haukupangwa kwenye ratiba iliyofanyiwa maboresho na kutangazwa Februari mwaka huu, ambapo sasa utachezwa saa 11:00 jioni, Yanga ikiwa mwenyeji.

“Klabu za Simba na Yanga pamoja na wadau wengine wa

INAENDELEA UKURASA 23

# Benchikha aweka wazi wakusajiliwa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikitolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu wa tano sasa, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ameweka wazi kuna kazi ya ziada inabidi kufanyika, ikiwamo kusajili washambuliaji wenye uwezo mkubwa wa kutumia nafasi zinazopatikana.

Simba jana ilirejea nchini ikitokea Misri ambapo ilikubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Al Ahly, hivyo kutupwa nje kwa jumla ya mabao 3-0 kutokana na mechi ya awali nyumbali katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kufungwa bao 1-0.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya kurejea nchini, Benchikha alisema pia kupoteza mchezo wa kwanza nyumbani dhidi ya Al Ahly uliongeza ugumu kwenye mechi ya marudiano, lakini akidai kuna mambo wamejifunza na kuahidi kuyafanyia kazi kwa msimu ujao ili kuwa bora zaidi.

Benchikha alisema Al Ahly ni timu bora na ina wachezaji wenye uzoefu ambao wanaweza kubadili mchezo muda wowote na hilo ndilo lililowagharimu, ikiwamo kupoteza nafasi nyingi kwenye mechi ya kwanza nchini.

“Lakini hatukuzitumia nafasi na wenzetu walipata moja pekee na waliitumia hiyo hiyo, ninaimani msimu ujao tukishiriki michuano hii tutakuwa bora zaidi kwa kuwa tutakuwa tumejifunza mengi, ikiwamo kuongeza baadhi ya wachezaji wenye uzoefu ambao wataongeza nguvu kwa waliopo hususan washambuliaji.

“Nafikiri kupoteza mechi ya kwanza nyumbani ndipo tulipoongeza ugumu wa mechi ya marudiano, Al Ahly ni timu bora na ina wachezaji wenye uzoefu wa michuano hii. Tumejifunza na naamini tutakuwa bora katika michuano hii mwakani kama tukipata nafasi ya kushiriki,” alisema Benchikha.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema hawajilaumu kwa kutolewa na Al Ahly katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika bali wamejifunza ili wakati mwingine washiriki wakiwa bora zaidi.

Alisema hawana ubovu huo unaotwajwa kwa sababu timu imeweza kufikia hatua ya robo fainali ambayo imezoeleka na sasa wanaenda kutengeneza utamaduni wa kucheza nusu fainali.

“Hakuna ubovu huo unaoimbwa, sasa tunaenda kutengeneza timu, nusu fainali si rahisi, lazima

INAENDELEA UKURASA 23



Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042